# Nipashe

Jumamosi Juni 20, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580263

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




## Mume ashikiliwa tuhuma kuua mkewe kikatili

UKURASA 3

# KILIO KATIBA MPYA

## LHRC yataka kufufuliwa mchakato, yadai kuna umuhimu kwa Watanzania...

*Endelea ukurasa 2*




Haji Rashid Pandu

Mwatum Mussa Sultan

Dk. Abdulhalim Mohamed Ali

Prof. Makame Mbarawa

## MWANAMKE AJITOSA URAIS ZANZIBAR WAFIKIA 13

UKURASA 3

## BAA LA CORONA



Unaweza kupunguza hatari ya kupata maambukizi au kuenea kwa Covid-19 kwa kuchukua tahadhari zinazotolewa na mamlaka zinazohusika. WHO

- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Wanaharakati wachambua utendaji Bunge la Jamhuri

UKURASA 2


MICHEZO SIMBA, MWADUI MECHI YA KISASI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Kilio Katiba mpya

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetaka kufufuliwa kwa mchakato wa Katiba mpya kutokana na kuona bado kuna umuhimu kwa Watanzania.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Anna Henga, katika mdahalo uliohusu umuhimu wa Katiba hiyo, uliofanyika jijini hapa.

Alisema bado Katiba ni kipaumbele kwa Watanzania na wataendelea kudai hadi itakapopatikana.

"Naamini mifumo yote nchini inahitaji Katiba mpya hata kama hautamaliza matatizo kwa asilimia 100, lakini itaonyesha mahali pa kuanzia," alisema.

Alisema hawakatishwi tamaa hata kama si kipaumbele kwa serikali, lakini ni kipaumbele kwa wananchi.

"Wananchi kwetu ndio kipaumbele, kwa hiyo serikali iliyopo na itakayokuwapo tutaendelea kuichagiza kuwa Katiba mpya lazima iwepo," alisema.

Alisema wameandaa mikutano mingi kuhusu Katiba mpya na wataendelea kuwa mchakato wake ulitumia fedha nyingi za Watanzania.

"Tusaidiane kuielimisha jamii kuwa Katiba mpya bado inahitajika na pia tunapoelekea katika uchaguzi wananchi wadai Katiba mpya," alisema.

Awali, akitoa mada kwenye mdahalo huo, mchambuzi wa masuala ya Katiba, Sera, Siasa, na Maendeleo ya Watu, Mchereli Machumbana, alisema kuna umuhimu wa kuwa na Katiba mpya kwa kuwa baadhi ya sheria zilizopitishwa na Bunge la 11 zinakinzana na Katiba ya sasa na hivyo kuhitaji msukumo wa kuendelea kuidai.

"Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 64(5), inalitaka Bunge kutunga sheria isiyokinzana na Katiba na endapo likitunga sheria inayokinzana na katiba, sheria hiyo itakuwa ni batili, kwa mfano Bunge limetoa kinga ya kupindukia kwa viongozi kushtakiwa," alisema.

"Upitishwaji wa sheria hizi unawataka wananchi kudai Katiba mpya kwa kuwa kumewekwa masharti ya mtu anayetaka kufungua shauri la kikatiba ni lazima aieleze mahakama ni kwa kiasi gani mlalamikaji ameathiriwa na ukiukwaji wa haki anayolalamikia, mfano ile kesi ya watoto chini ya miaka 18 kuolewa kwa mabadiliko haya hana nafasi ya kufunga shauri tena," alisema.

Alisema umma wa Watanzania unapaswa kuendelea kufuatilia na kutambua haki zao kikatiba zinazopaswa kulindwa kwa mujibu wa sheria.

Mwaka 2010 Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, alitangaza nia ya kuanza mchakato wa Katiba mpya, na mwaka 2011 ulianza kwa kutunga sheria ya mabadiliko ya katiba na baadaye kufuata sheria ya kura ya maoni.

Kutokana na sheria hiyo, iliundwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoratibu mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi na kuandaa rasimu ya kwanza iliyohaririwa na mabaraza ya Katiba na kupata rasimu ya pili iliyowasilishwa kwenye Bunge Maalum la Katiba.

Mwaka 2014 Bunge lilijadili na kutoka na Katiba inayopendekezwa na kubaki hatua ya kura ya maoni ambayo kwa mujibu wa sheria ilipangwa kufanyika Aprili 30, mwaka 2015.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais mpya wa Burundi Evariste Ndayishimiye, Ikulu ndogo Gitega nchini Burundi juzi. Makamu wa Rais alimwakilisha Rais Dk. John Magufuli katika hafla ya kumwapisha rais huyo. Kushoto ni Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete. **PICHA: OMR**.

## Wanaharakati wachambua utendaji Bunge

**Na Waandishi Wetu**

WANAHARAKATI, wasomi na wananchi wamechambua kuhusu utendaji wa Bunge la 11 na kueleza mambo mazuri yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha utendaji.

Baadhi ya wanaharakati hao wamesema bunge hilo lilifanyakazi nzuri kwa mujibu wa Katiba na wengine wamelikosoa kwa kupitisha sheria zilizokinzana na Katiba ya nchi.

Mchambuzi wa masuala ya Katiba, Sera, Siasa na Maendeleo ya Watu, Mcheleli Machumbana, alisema kwa miaka mitano ya Bunge la 11 lilikuwa na upitishaji wa sheria zinazokinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kwa mfano Bunge limeweka kinga ya kupindukia kwa viongozi wakuu wa nchi kushtakiwa, suala ambalo linatuhitaji kudai Katiba mpya kwa kuwa sheria ya namna hii inaondoa dhana ya usawa," alisema.

Alisema Katiba inalitaka Bunge kutunga sheria isiyokinzana na Katiba na kama ikitungwa sheria ya namna hiyo itakuwa ni batili.

**THRDC-BUNGE HALIKUWAJIBIKA**

Mkurugenzi wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema jukumu kubwa la Bunge kwa mujibu wa Katiba sura ya 62-64, ni chombo cha uwakilishi, kuiwajibisha, kuisimamia, kuishauri serikali na kutunga sheria.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ya Bunge la 11 katika eneo la uwakilishi kama sehemu ya jukumu la Bunge, halikufanya kazi hiyo bali ilikuwa ni sehemu ya kutetea mhimili mwingine ambao ni serikali.

"Ukiniambia Bunge limefanya kazi kiasi gani ni lazima yaguswe maeneo hayo matatu, katika eneo la uwakilishi, kipindi chote cha miaka mitano ikilinganishwa na mabunge yaliyotangulia, hili halijatimizwa na badala yake lilikuwa sehemu ya uwakilishi wa serikali," alisema Olengurumwa.

Alisema mwenendo wa Bunge ulivyokuwa wakati mwingine Spika alikuwa akizungumza kama Bunge limeungana na serikali, hivyo wananchi walikosa watu wa kuwatetea.

Kuhusu suala la kusimamia na kupitisha mabadiliko ya sheria, Olengurumwa alisema hilo halikusimamiwa kwa sababu Bunge lilipitisha mabadiliko ya sheria mbalimbali bila kuwashirikisha wawakilishi kikamilifu.

"Bunge la 11 ni wakati ambao limepitisha sheria kali mbalimbali bila kuwashiriki wawakilishi. Sheria hazitungwi kwa manufaa ya nchi," alisema Olengurumwa.

Alisema Bunge hilo likilinganishwa na mabunge mengine yaliyotangulia, limeshindwa kuunda kamati za kushughulikia masuala makubwa ya nchi.

Alitoa mfano sakata la Richmond na Escrow kama mambo ambayo yalijadiliwa katika mabunge yaliyopita ambayo yalikuwa na maslahi mapana kwa taifa, lakini kwa Bunge la 11 hakukuwa na suala kubwa la kushughulikiwa.

**SERIKALI ILIFURAHI**

Mchambuzi wa masuala ya siasa za Tanzania, Deusi Kibamba, alisema kikubwa kilichofanyika kwenye bunge hilo ni kutokwamisha miswada yote iliyokuwa ikipelekwa.

"Ninaamini kwamba serikali ya awamu ya tano itakuwa imefurahi sana, hili ni bunge ambalo limeisaidia kwa kiwango kikubwa kufanya shughuli zake kwa sababu karibu kila mswada uliokuwa ukipelekwa, ulikuwa unapitishwa tofauti na ilivyokuwa katika mabunge mengine yaliyopita," alisema Kibamba.

"Nafikiri hili lilisababishwa na kasi iliyokuwa inaendeshwa katika serikali ya awamu hii ambayo wakati mwingine ilionekana kuwa mbele kuliko ya bunge."

**BUNGE 'LIVE'**

Mkurugenzi wa Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC), Theodosia Nshala, alisema Bunge la 11 liliwanyima wananchi fursa kufuatilia utendaji wa wabunge wao baada ya kubadilisha utaratibu uliokuwa ukifanyika kipindi cha nyuma kwa kurusha matangazo yake mubashara kupitia vyombo vya habari.

Pia, alisema utaratibu wa kutokurusha matangazo hayo, ulichangia Bunge kuonekana halina mvuto kwa wananchi na walikata tamaa kufahamu kinachoendelea.

"Mbali na Bunge la 11, mengine yote yalikuwa yanaonyeshwa mubashara wakati wote, lakini hili lililopita lilibadilisha utaratibu wake na kuwanyima fursa wananchi kufuatilia kile wabunge wao wanachowawakilisha, kwa hiyo baadhi ya wananchi ambao walikuwa hawana uwezo wa kufuatilia katika vyombo vya habari hawakupata kabisa taarifa za bunge," alisema Nshala.

"Kwa namna moja ama nyingine, watu wengine walikosa fursa ya kuona au kufuatilia kile kilichokuwa kikiendelea katika bunge hilo."

Alipendekeza Bunge lijalo liboreshe zaidi utaratibu wake hususani kwa kurudisha utaratibu huo wa kuonyeshwa mubashara.

"Ni bora liwe 'live' ili watu wafuatilie na kujifunza, na kuona kama je, wale waliowatuma wanafanya kile kweli walichotumwa?" Alishauri Nshala.

Naye, Kibamba alisema bunge hilo kubadilisha utaratibu wa kurusha matangazo mubashara, kulipunguza kasi ya utendaji kwa baadhi ya wabunge.

"Kipindi bunge linaonyeshwa 'live', lilikuwa linasaidia kila mbunge kufanya kazi ya kuwawakilisha wapigakura wake kwa bidii kwa sababu walikuwa wanaogopa kwamba wanafuatiliwa," alisema Kibamba.

"Wabunge walikuwa wanajitahidi asiposimama na kuchangia angalau wanaona bora waandike ili ijulikane kwamba na wao wanachangia, lakini katika bunge hilo la 11 walikuwa hawajali," alisema Kibamba.

Akizungumzia namna anavyoliona bunge lijalo, Kibamba alisema anatarajia litakuwa gumu zaidi kwa sababu litakuwa linaelekeza nguvu zaidi katika kufikiria aina ya uongozi wa awamu nyingine ya serikali itakayofuata.

Pia, alisema anatarajia litakuwa gumu zaidi kwa sababu anaamini litakuwa na wabunge wengi zaidi wa chama kimoja kuliko mabunge yote.

***Imeandikwa: Mary Geofrey na Elizabeth Zaya (DAR), Augusta Njoji na Paul Mabeja (DODOMA)***

# Mwanamke ajitokeza kuwania urais Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**




MCHUANO wa kumrithi Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein umepamba moto visiwani Zanzibar baada ya jana makada wanne kujitokeza kuchukua fomu ya kugombea urais akiwamo mwanamke wa kwanza kuonyesha nia hiyo visiwani humo.

Makada hao wanaungana na wengine tisa ambao wameshachukua fomu hizo na kufanya idadi ya waliochukua fomu ya kuwania nafasi hiyo kuwa 13.

Majira ya saa 5:14 asubuhi jana, mwanamke wa kwanza alijitokeza kuchua fomu ya kuwania nafasi hiyo.

Akizungumza na wandishi wa habari, Mwatum Mussa Sultan (pichani), alisema ameamua kuchukua fomu ili kuwapa hamasa kinamama wenzake kujitokeza kugombania ili kufikia asilimia 50 kwa 50 ya uongozi.

Alisema wanawake wana wajibu wa kugombe nafasi za uongozi ikiwamo urais, ubunge, uwakilishi na udiwani.

Alisema, ikiwa wanawake hawatajitokeza kugombea nafasi hizo hawatafikia asilimia hiyo.

Aliwataka wanawake wenzake kutoogopa kugombea nafasi ya urais kwa sababu CCM ni chama cha watu wote.

Alikipongeza chama kwa kuweka uwazi na demokrasia kwa waanchama wa CCM kuchukua nafasi yoyote kugombea bila kuchagua jinsia.

Aliwapongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Magufuli kwa kutekeleza vyema ilani ya chama ambayo Watanzania wameshuhudia.

Mwanachama mwingine aliyejitokeza kuchua fomu ni Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, Waziri wa Maji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye alifika ofisi kuu ya chama majira ya saa 3:56 asubuhi.

Alisema, kitendo cha kuchukua fomu ni tukio la kihistoria katika maisha yake na kuwaomba wananchi na Watanzania kuendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu na kuwasimamia kwa kila hatua.

"Ndani ya moyo wangu natamani nizungumze nanyi, lakini nakuombeni leo wanahabari tusizungumze mengi tunakwenda kazini tunaomba Watanzania waendelee kutuombea kwa Mwenyezi Mungu atusimamie na kutufanya wepesi katika safari hii...dua zenu ni muhimu, katika kufungua milango," alisema.

Majira ya saa nane mchana, Haji Rashid Pandu ambaye ni mkulima, alichukua fomu na kueleza uamuzi wake unatokana na kutaka kuleta mapinduzi ya kilimo kupitia sekta ya hiyo kilimo. Alisema, pamoja na maisha ya wananchi wa Tanzania kutegemea kilimo, bado kuna kazi ya kufanya hivyo iwapo atateuliwa na CCM na wananchi wa Zanzibar kumpa ridhaa, atahakikisha sekta hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Zanzibar na watu wake.

Saa 8:30 mchana, Alhaj Dk. Abdulhalim Mohammed Ali alichukua fomu na kuwaomba wananchi wa Zanzibar kujenga matumaini kwake pale atakapopata ridhaa ya chama na Wazanzibari kuhakikisha anaendeleza palipoachwa na viongozi wengine katika kusukuma mbele maendeleo ya Zanzibar.

Hadi jana watia nia 13 walikuwa wachukua fomu akiwamo, Mbwana Bakari, Balozi Ali Karume, Mbwana Mwinyi Yahya, Omar Shehe, Muhammed Jafar, Muhammed Hija, Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor, Shamsi Vuai Nahodha, Dk. Hussein Mwinyi, Profesa Makame Mbarawa, Mwatum Mussa Sultan, Haji Rashid Pandu na Dk. Abdul-halim Mohammed Ali.

Makada wote hao walikabidhiwa fomu za kugombea nafasi ya urais na Katibu wa Idara ya Oganaizesheni ya kamati maalum ya CCM Zanzibar, Galous Nyimbo.

# Mkazi Dar atuhumiwa kumuua mkewe

**Na Romana Mallya**

MKAZI wa Kimara Stop Over jijini Dar es Salaam, Erick Bubelwa, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuua mke wake wa ndoa kikatili, Mercy Mkambala (30), kisha kumpeleka hospitali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Edward Bukombe, aliiambia Nipashe jana kuwa tukio hilo lilitokea Jumanne saa 11 alfajiri nyumbani kwao maeneo ya Kimara Stop Over.

Alisema wanamshikilia mume wa marehemu kwa sababu inadaiwa ndiye aliyemshambulia kwa kumpiga na kitu chenye ncha kali kwenye paji la uso na kusababisha kifo chake.

"Ni kweli hilo tukio limetokea Juni 16, mwaka huu huko Kimara na tayari Jeshi la Polisi linamshikilia mume wa marehemu kwa kumshambulia mke wake, yeye ndiyo chanzo cha kifo chake," Kamanda alisema.

Mmoja wa majirani (hakupenda jina lake litajwe) alisema aliamshwa na mume wa marehemu usiku wa tukio kuomba msaada.

Alisema mume huyo alidai mke wake, amejigonga kwenye meza na kudondoka chini na kupasuka hivyo kuvuja damu nyingi.

"Tulipofika nyumbani kwao, badala ya mume kuingia ndani alirudi eneo la geti, tulipomuhoji mbona anarudi getini badala ya kuingia ndani, alitueleza anakwenda kutafuta usafiri, hivyo hatukuweza kuingia ndani tuliendelea kusimama nje hadi aliporudi na bodaboda."

Jirani huyo alidai mume wake alimuhoji mtuhumiwa kama usafiri aliokuja nao mgonjwa anaweza kupanda ndipo alipojibiwa hapana.

"Tulikubaliana aende kutafuta gari na aliondoka na baada ya muda lilikuja gari aina ya Allex na ndipo tulipoingia chumbani kwa msaada wa mwongozo wa msaidizi wa ndani.

"Wakati huo ilikuwa giza umeme ulikuwa hakuna, tulipoingia chumbani tulimkuta Mercy akiwa amelala kitandani akitokwa na damu nyingi eneo la kichwani na alikuwa hajavaa nguo hivyo tulimsitiri kwa khanga ndipo wanaume walimbeba hadi kwenye gari."

Alisema waliondoka watu watatu ambao ni mume wa marehemu, dereva ambaye ni mdogo wa marehemu na jirani kuelekea hospitali ya Bhoch iliyopo Kimara.

Alisema baada ya muda majira ya saa tisa usiku taarifa zilirudi kuwa vipimo vya daktari vimeonyesha Mercy amefariki dunia.

Mdogo wa mtuhumiwa, Anna Kurwa, alisema kuwa alifika nyumbani kwa kaka yake kuwasalimia na wakati tukio likitokea alikuwa ndani.

"Tulipoingia ndani (chumbani) kwa kweli kile kitendo kilichofanyika pale hapana, dada alikuwa na majeraha kwenye paji la uso na alivuja damu sana.

"Mpaka sasa swali ninalojiuliza ilikuaje na mbaya zaidi hatukusikia kelele yoyote kwamba kuna nini ili tutoke tuangalie kuna shida gani, kiukweli yule dada ameumia na ameteseka sana hadi kufikia umauti."

Mama mdogo wa marehemu, Aglipina Dominic, alisema mama wa marehemu alimpigia simu kumjulisha kuwa, amepokea taarifa kuwa Mercy kapigwa na shoti ya umeme chumbani kwao.

"Alijulishwa kuwa shoti ilitokea chumbani akakimbilia sebuleni na akajigonga kwenye meza na kupasuka kichwa damu zinamtoka nyingi na wakati anakimbizwa hospitali akafariki dunia," alisimulia.

Alisema baada ya kufika eneo la tukio walikuta mlango umefungwa na askari walikuwa wameshakuja na baadaye jioni ulipofunguliwa, hali ya sebule walibaini siyo kweli kama walivyosimulia ikilinganishwa na hali waliyoikuta chumbani.

"Zile damu tulizozikuta kwenye shuka, mito ni kama kitendo kingetendeka sebuleni haya makochi tungekuta yamedondokewa na damu nyingi, lakini hatukukuta chochote sebuleni. Wanandoa hawa walifunga ndoa miaka miwili iliyopita," alisema.

Mama mkubwa wa marehemu, Letisia Kantunzia, alisema Mercy aliwahi kumweleza mdogo wake kuwa, endapo atafariki azikwe upande wa wazazi wake na siyo wa mume wake.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UWEKAJI WAZI DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi kuwa itaweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa siku nne kuanzia tarehe 17 hadi 20 /06/2020, katika vituo vilivyotumika wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la wapiga Kura. Uwekaji wazi huu utafanyika kwa kuzingatia tahadhari zote za afya kuhusu kuzuia maambukizi ya ugonjwawa COVID-19 unaosababishwa na Virusi vya Corona.

**Uboreshaji utafanyika kama ifuatavyo :-**

1. **SIKU** : Uwekaji wazi utafanyika tarehe 17-20/06/2020
2. **VITUO** : Uwekaji Wazi utafanyika katika Kituo kilichopangwa kwenye kila Halmashauri husika.
3. **MUDA** : Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uwekaji Wazi utahusisha.**

- Wapiga Kura wote walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2015, walioandikishwa wakati wa Uboreshajiwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na ya Pili kwa Mwaka 2019/2020.
- Wapiga Kura hawa ni wale ambao hawakuhakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura awamu ya kwanza.
- Wapiga kura watakaohakiki taarifa zao kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura lilipowekwa wazi na kukuta picha zao hazipo wanatakiwa kwenda kwenye ofisi za Halimashauri ili wapigwe picha nyingine na kupewa kadi..

**Utaratibu wa Uhakiki.**

Mpiga kura anaweza kuhakiki taarifa zake kwa njia zifuatazo:-

1. Mpiga Kura mwenyewe kufika katika kituo alichojiandikisha na kuhakiki taarifa zake katika orodha itakayokuwa imebandikwa katika kituo hicho. Mtu mmoja kwenye familia anaweza kukagua taarifa za familia nzima.
2. Mpiga Kura kupitia simu yake ya kiganjani kupiga namba *152*00# na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
3. Mpiga kura kupiga simu namba 0800112100 na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
4. Mpiga Kura kuhakiki taarifa zake kupitia Tovuti ya Tume, www.nec.go.tz kwa kubonyeza sehemu iliyoandikwa 'uhakiki' na kuendelea kufuata maelekezo.

**Mambo ya kuzingatia.**

1. Daftari la awali la wapiga kura litabandikwa katika vituo vyote vilivyotumika kuandikisha wapiga kura.
2. Iwapo mpiga Kura amehakiki taarifa zake kwa kutumia njia yoyote kati ya hizo nne na kutaka kufanya marekebisho ya taarifa zake atatakiwa kwenda katika Ofisiza Halmashauri husika na kufanya marekebisho hayo.
3. Mpiga Kura anayehitaji kumuwekea pingamizi Mpiga Kura asiye na sifa zakuwemo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura ataenda katika Kituo kilicho pangwa kwenye Halmashauri husika.
4. Wapiga kura wanatakiwa kutoa taarifa za ndugu waliofariki dunia ili waondolewe kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
5. Katika zoezi hili hakutakuwa na Uandikishaji wa Wapiga Kura Wapya. Aidha, hakutakuwa na Uboreshaji wa Taarifa za Wapiga Kura waliohama maeneo yao ya kiuchaguzi, waliopoteza kadi au kadi zao kuharibika.

**Muhimu:** Kumbuka kuzingatia Kanuni za Afya kwa kufuata Maelekezo utakayopewa kituoni ili kujiepusha na maambukizi ya Virusi vya Corona

Dkt. Wilson Mahera Charles
MKURUGENZI WA UCHAGUZI

2157775002

**Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar Es Salaam, Tel.+255 22 2114963-6. Nukushi: +255 22 2113382. Barua Pepe: info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.**

# Samia kupokea matembezi kumpongeza JPM

**Na Hellen Mwango**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassani leo anatarajia kupokea matembezi ya Shirikisho la Vyama vya Madereva Pikipiki na Bajaji wa Mkoa wa Dar es Salaam (Bodaboda Appreciation Tour For JPM 2020) ya kumpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa kutekeleza miradi katika kipindi chake cha miaka mitano.

Akizungumza na waandishi wa habari Kivukoni jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Edward Mwenesongole, alisema matembezi hayo yameratibiwa na Robart Makonyo kwa lengo la kumpongeza Rais Magufuli kwa uzalendo wake.

Matembezi hayo yataanzia kupitia miradi hiyo ikiwamo Daraja la Tanzanite, Daraja la Mfugale (Tazara), Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, kituo cha kufua umeme Kinyerezi, stendi ya mabasi Mbezi na Daraja la Ubungo Interchange na kupokelewa na Mama Samia viwanja vya Urafiki jijini Dar es Salaam.

"Shirikisho letu limeridhishwa na kazi ya miaka mitano na jitihada za Rais Magufuli katika kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), tutafanya matembezi hayo kesho (leo) yatapokelea na Makamu wa Rais viunga vya Urafiki jijini Dar es Salaam," alisema Mwenesongole.

Akifafanua, alisema salamu za pongezi zitapokelewa na Mama Samia kwa kuwa wamefanya kazi pamoja na kufanikisha miradi mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Naye Mhazini wa shirikisho hilo, Saidi Kagoma, alisema madereva wa bodaboda na bajaji jijini Dar es Salaam, walikuwa wananyanyasika, lakini chini ya Mkuu wa Mkoa, Paul Makonda ajira yao imekuwa na amani bila bugudha.

"Tulikuwa tunanyanyasika kukamatwa ovyo ovyo, lakini Mkuu wa Mkoa Makonda amepiga marufuku tusikamatwe tunaingia mjini kufanya shughuli zetu za utafutaji wa mkate wa kila siku bila vikwazo," alisema Kagoma.

Alisema wanajivunia maendeleo ya miradi mikubwa na barabara kwa miaka mitano ya Rais Magufuli ambayo imewasaidia kufanya kazi kwa urahisi ikiwamo sehemu zenye madaraka kutokana na kuondoa kero za foleni jijini.

# Serikali yasaidiwa vifaa zaidi bil. 2/-

**Na Zuwena Shame**

SERIKALI imepokea vifaa tiba na kinga venye thamani ya Sh. bilioni 2.9 kutoka kwa taasisi za serikali, binafsi na mashirika ya maendeleo.

Misaada hiyo ilipokelewa jijini Dar es Salaam jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Akipokea msaada huo, Prof. Makubi, alisema vifaa kinga na tiba vitasaidia utoaji bora wa huduma nchini kwa kusambazwa katika zahanati na vituo vya afya nchini.

Alisema serikali ikishirikiana na TAMISEMI imeongeza vituo vya huduma za afya nchini kutoka 7,014 hadi 8,783 na zahanati mpya 487 kwa muda wa miaka mitano.

Alisema serikali imejipanga kuimarisha vituo vya kanda na mikoa hivyo huduma bora zinahitajika ili kupunguza changamoto mbalimbali za kiafya ikiwamo vifo vya mama na mtoto nchini.

Alitoa mfano wa baadhi ya misaada hiyo kama vitanda na vifaa vya chumba cha uangalizi maalumu (ICU) vya wagonjwa ambavyo vilikuwa vinahitajika kwa upande wa huduma za afya.

Ofisa Mradi wa Shirika la Plan International nchini, Peter Mwakabwale, alisema kusudio la kutoa msaada huo ni kuisaidia serikali upande wa huduma za afya hasa wafanyakazi na watoa huduma nchini ili kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mwakabwale alivitaja baadhi ya vifaa hivyo kuwa ni vipimia joto, miwani tiba, nguo za kazi, vitakasa mikono, barakoa, viatu na glovu vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 38.

"Kupitia mpango huu na vifaa hivi tuna uhakika changamoto za kiafya kwa watoa huduma wa afya zitatatuliwa kwa kuwa watatoa huduma kwa ubora na uhakika," alisema.

Alisema Shirika la Plan litaendelea kusaidia serikali katika nyanja mbalimbali ikiwamo afya ili kuhakikisha maisha ya wananchi yanalindwa hasa haki za watoto wa kike ambao wanaonekana kuathirika zaidi.

Baadhi ya taasisi za umma na binafsi na mashirika yaliotoa misaada mbalimbali ni pamoja na Benki ya I&M, Plan International, KOICA, Wakala wa Vipimo Nchini (WMA), Kioo Limited, Stanbic Bank, Bohari ya Dawa (MSD), Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC) na TICTS.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Rejareja cha Benki ya I&M, Lilian Mtali, akionyesha mfano wa kunawa mikono, baada ya kukabidhi matangi matano yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusaidia watu kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aliyeshtakiwa kumwibia mbunge aachiwa huru

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Mwanzo Maromboso jijini hapa, imemwachia huru mfanyakazi wa ndani, William Mlewa, aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya wizi wa shilingi milioni saba za mwajiri wake, Anjela Kizigha, mbunge wa zamani wa Bunge la Afrika Mashariki baada ya kumkuta hana hatia.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu wa Mahakama hiyo, Neema Mchomvu, alisema ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka umeshindwa kujitosheleza kuishawishi mahakama hiyo kumtia hatiani mshtakiwa.

Alisema mashahidi sita wa upande wa mashtaka wameshindwa kuthibitisha mashtaka, hivyo mahakama imeona mshtakiwa hana hatia na kumwachia huru.

Awali, mlalamikaji wa shauri hilo, Kizigha, aliiambia mahakama hiyo kuwa mshtakiwa, alikuwa mfanyakazi wake wa ndani kwa nyakati tofauti na alimwibia kiasi hicho cha fedha na baada ya tukio hilo, alijizuru kwa kujitumbukiza kwenye sufuria la uji wa moto kwa lengo la kupoteza ushahidi.

Hakimu Mchomvu alidai kuwa upande wa mashtaka unaweza kukata rufani ndani ya siku 30 kama haujaridhika na uamuzi wa mahakama hiyo.

# Mbunge Kishapu alipa faini akwepa jela

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Jimbo la Kishapu mkoani Shinyanga, Suleiman Nchambi (CCM) na wenzake wawili wamekiri makosa na kulipa faini ya Sh. milioni 32.5.

Washtakiwa hao walilipa faini hizo baada ya kukiri makosa ya uhujumu uchumi na kukwepa kwenda jela.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga, Ushindi Swalo.

Kesi hiyo ilisikilizwa kwa njia ya makubaliano baada ya watuhumiwa kumwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaki Nchini (DPP), kukiri makosa yao na kuomba kulipa faini.

Katika hukumu hiyo, Nchambi aliyekuwa anakabiliwa na makosa tisa alitakiwa kulipa Sh. milioni 22.5 au kwenda jela miezi mitatu kwa kila kosa.

Mshtakiwa wa pili Yahya Soud, aliyekuwa anakabiliwa makosa manne alitakiwa kulipa Shilingi milioni saba au kwenda jela mwaka mmoja, naye alilipa fedha hizo.

Mshtakiwa wa tatu, Abdala Soud, alikuwa akikabiliwa na makosa mawili, alitakiwa kulipa faini ya Shilingi milioni tatu au kwenda jela mwaka mmoja, naye alilipa faini hiyo.

Baada ya kulipa faini hizo mahakama iliwaachia huru washtakiwa wote.

Mbunge huyo alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza Mei 8, mwaka huu, akikabiliwa na kesi namba 10, 2020, na kusomewa mashtaka 12 ya uhujumu uchumi, kwa kumiliki bunduki na risasi kinyume na sheria.

# Mwalimu Mkuu akutwa kajinyonga hadi kufa

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Chisegu, Halmashauri ya Mji wa Masasi, mkoani Mtwara, Mohamedi Mboloma, amekutwa amejinyonga msituni baada ya kutoweka nyumbani kwake kwa siku tatu bila kuaga.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo wakati akiongea na Nipashe jana, ofisa wa Jeshi la Polisi ambaye hakutaka jina lake litajwe kwa kuwa sio msemaji, alisema tukio hilo limegundulika jana katika msitu huo uliopo nje kidogo ya kijiji cha Mbaju, Kata ya Chigugu huku mwili ukiwa juu ya mti ukining'inia.

Alisema mwalimu huyo ambaye ni mwenyeji wa Mtwara mjini, anadaiwa kabla ya kufanya uamuzi huo alitoweka nyumbani kwake kwa siku tatu bila ya kuaga wala kutoa taarifa kwa familia yake.

Alisema inadaiwa kuwa alitoweka nyumbani tangu Juni 16, saa 10 jioni akiwa na gari lake dogo na kuelekea katika matembezi yake kama kawaida na hakuonekana tena hadi mwili wake ulipokutwa ukining'nia msituni.

Alisema mwalimu huyo amekutwa akiwa amejinyonga kwa kutumia mkanda wake wa suruali pamoja na kamba na kwamba alikwenda katika msitu huo na kuliacha gari lake kando na kujinyonga.

"Marehemu alifika huku akiwa na gari lake na inaonekana baada ya kufika hapa aliweka simu zake zote mbili ndani ya gari na kufunga milango ya gari kisha kuingia msituni na kutimiza azma yake hiyo ya kujinyonga," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi baada ya kupata taarifa ya kupotea kwa mwalimu huyo na baadaye kuonekana gari lake likiwa karibu na msitu huo, lilifanya msako katika msitu huo.

Alisema msako huo ulifanyika jana kwa kushirikiana na wanakijiji wa kijiji hicho kwa kuingia ndani ya msitu huo kutamfuta, lakini hata hivyo hawakuweza kumpata.

Alisema, jana wananchi waliingia tena msituni, lakini upande wa pili ndipo walipokuta mwili huo wa marehemu ukiwa juu ya mti ukining'inia.

Alisema jeshi hilo linachunguza chanzo cha mwalimu huyo kujinyonga na upelelezi unaendelea.

Alisema polisi wameshautoa mwili kwa ajili ya kuwakabidhi ndugu zake ili waendelee na taratibu zingine za mazishi.



Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohamed Bakari (kushoto), akipokea msaada wa vitakasa mikono vyenye thamani ya Sh. milioni 25 kutoka kwa Meneja Utawala wa Kioo Ltd, Kapil Dave, katika hafla iliyofanyika ofisi za Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mshauri wa masuala ya Afya wa kampuni hiyo, Richard Msumule . **PICHA: MIRAJI MSALA** .

# Mwendesha bodaboda adaiwa kuwaingilia watoto kwa zamu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MWENDESHA bodaboda aliyefahamika kwa jina moja la Kamala, mwenye umri unaokadiriwa kuwa kati ya miaka 25 na30, anatafutwa na polisi kwa tuhuma za kubaka kwa zamu watoto wawili wenye umri wa miaka minane na tisa.

Imedaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa akiwalaghai watoto hao kwa kuwapa Sh. 1,000 kila mmoja.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Revocatus Malimi, alisema mtuhumiwa anadaiwa kutenda makosa hayo kwenye jengo la nyumba ambayo halijakamilika kwa kuwaingilia kimwili kwa zamu.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, watoto hao ni wanafunzi wa shule ya msingi mmoja akiwa darasa la pili na mwingine la tatu.

"Walifanyiwa kitendo na mtuhumiwa kwa kuwashawishi kufanya tendo hilo na kuwapa Sh. 1,000 kila mmoja za kununulia urembo aina ya bangili za mikono kila anapowaingilia kingono," alisema Malimi.

Alisema taarifa za watoto hao kuingiliwa ziligundulika baada ya kuwaeleza watoto wenzao waliowaona wamevalia bangili hizo wazizonunua kutokana na fedha hizo.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, mazungumzo ya watoto hao yalimshtua mama wa jirani kwenye eneo ambalo walikuwa wakicheza na kumfanya awaendee kwa upole na kuwauliza ndipo bila uoga walimsimulia kila kitu.

"Yule mama aliyekuwa anasimuliwa tukio hilo alimwendea mzazi mmoja wa watoto hao na kumsimulia kisha kuripotiwa polisi na kuanza uchunguzi wa awali," alifafanua Malimi.

Kamanda alisema mtuhumiwa huyo hajafahamika eneo analoishi, lakini eneo hilo hutumia kuegesha bodaboda yake na alitumia mbinu ya kuwafuata watoto hao wanapocheza na kuwaita pembeni.

Alibainisha kuwa kutokana na watoto hao kumwona mara kwa mara eneo hilo walimsogelea na kumsikiliza na kumkubalia ndipo akawapeleka ndani jengo kuwaingilia kwa zamu.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta mtuhumiwa na kumtaka ajisalimishe kabla ya serikali haijaweka mikono wake.

# Maambukizi kichocho, minyoo yafikia asilimia 30

**Na Happy Severine,** SIMIYU

SHIRIKA la World Vision Tanzania, limesema kuwa kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa kichocho na minyoo ya tumbo wilayani Itilima mkoani Simiyu kimefikia asilimia 30.

Imeelezwa sababu ya hali hiyo ni uhaba wa upatikanaji wa majisafi na mazingira salama wilayani humo.

Asilimia hiyo ya maambukizi imebainishwa kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mwakilishi wa World Vision Tanzania, Rose Liwa, aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mradi wa kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele.

Alisema shirika hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea (KOICA), itahakikisha inawafikia walengwa 283,972 na kuyatokomeza kabisa magonjwa hayo.

Aliongeza kuwa kati ya walengwa hao, ndani yake kutakuwapo na kata 22, vijiji 102, vitongoji 587 na kaya 44,171 ambazo shughuli mbalimbali za utoaji dawa za minyoo na kichocho zitafanyika, uchimbaji na usambazaji maji kwa vijiji 10 na uhamasishaji wa usafi wa mazingira kupitia viongozi wa maeneo husika na matumizi ya vikundi vya sanaa.

Dk. Irene Mbugua, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa World Vision Tanzania, Gilbert Kamanga, alisema nguvu kubwa itaelekezwa kwenye magonjwa yasiyopewa kipaumbele watafanikiwa kuyatokomeza.

Naye, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Itilima, Dk. Arnold Musiba, alisema hali ya magonjwa hayo siyo nzuri kutokana na jamii kubwa ya wakazi wa wilaya hiyo kuwa na imani potofu ya dawa zitolewazo za minyoo na kichocho.

"Hali sio nzuri sana ingawa tumejitahidi kufanya kampeni mbalimbali za utoaji wa dawa hizo, lakini bado kuna wazazi wanawakataza watoto wao wasizitumie," alisema Dk. Musiba.

Alisema hali ya upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira ndani ya wilaya hiyo ndio sababu kuu ya maambukizi hayo kuwa juu kwa kuwa wakazi wengi hutumia maji ya madimbwi na mabwawa ambayo hayapo katika mazingira safi na salama.

Mradi huo wa miaka mitatu utagharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 864,993.00 sawa na Sh. bilioni 1.9.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashabiki, viongozi wa soka msiipuuzie corona

**BAADA** ya serikali kutangaza kurejesha michezo hapa nchini, swali na kilio kikubwa cha wadau kilikuwa ni kuruhusu mashabiki kuingia viwanjani kushuhudia michezo hiyo.

Ruhusa hiyo iliyotolewa na Rais, Dk. John Magufuli, ilikuwa si kwa ajili ya kumalizia msimu wa mwaka 2019/20, bali kukamilisha kalenda za mashindano mbalimbali yaliyokuwa yameshaanza.

Lengo kuu la kuruhusu michezo hiyo, ilikuwa ni kupata bingwa wa uwanjani badala ya mezani, na vile vile kutoa fursa ya shughuli za kiuchumi zilizokuwa zinafanyika kupitia mechi za Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi Kuu ya Wanawake ziendelee.

Hata hivyo kwa sababu bado hali haijawa shwari, Rais Magufuli aliwataka wadau wote wa michezo kuendelea na michezo hiyo, lakini wakifuata mwongozo kutoka kwenye Wizara ya Afya kuhusiana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona (Covid -19).

Hii ilikubaliwa kwa sababu serikali ilitaka kuona wanamichezo wanakamilisha mashindano na kalenda zao bila migogoro kama ilivyotokea kwa baadhi ya nchi kutangaza kufuta ligi na kutangaza mabingwa wakati msimu haukukamilika.

Hata hivyo, Nipashe imeshuhudia baadhi ya mechi za kirafiki na za ligi zikichezwa huku mwongozo kuhusiana na kujikinga na corona ikikiukwa.

Uamuzi huu wa kutofuata mwongozo, si tu utaziathiri timu husika ambazo zitafungiwa kucheza mechi zao mbele ya mashabiki na wanachama wao, pia zitawaweka katika hali hatarishi washangiliaji hao.

Bado Watanzania tunakumbushwa kuwa corona ipo na ni muhimu tuishi kwa kufuata tahadhari zote zinazoelekezwa na wataalamu wa afya ili kujiweka katika mahali salama.

Kuruhusu mashabiki kuingia viwanjani, isije kuwa ndio sababu ya mashabiki, wachezaji na wasimamizi wa michezo kujiweka kwenye hali ya hatari, wakati bado taifa linawategemea katika ujenzi wa taifa.

Viongozi wa klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Bara mnakumbushwa kufuata maelekezo na kamwe wasiangalie suala moja la mapato ya milangoni.

Tayari tumeshuhudia serikali kuifungia JKT Tanzania kucheza mechi zake za Ligi Kuu Bara bila mashabiki, na hii imetokana na viongozi wake kudaiwa kwenda kinyume na maelekezo wakati walipowakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Ruhusa hii iliyotolewa isitumiwe vibaya, mashabiki wanatakiwa kufuata maelekezo na kutolazimisha kutaka kuingia uwanjani pale wanapotangaziwa tayari uwanja umejaa.


Lazima wadau wa soka na michezo mingine wa hapa nchini, kukumbuka kwamba kuna maisha baada ya michezo, familia na wazazi wanawategemea, na endapo watateketea kwa ugonjwa huo, watawaletea shida wategemezi wao.

Kama imewezekana kwa kiasi kikubwa kupambana na ugonjwa wa malaria na vifo kupungua, vile vile inawezekana kwa kujikinga dhidi ya corona kwa kufuata taratibu na mwongozo kutoka katika Wizara ya Afya.

Hakuna kisichowezekana, kikubwa ni kufuata ushauri na mambo yatakwenda vizuri, timu na mashindano yaliyosimama wakati ugonjwa huo ukisambaa kwa kasi yatamalizika huku mashabiki wakibakia salama.

Ni wakati wa kila shabiki kukubaliana na kujiongoza mwenyewe na kamwe kuacha kusubiri kusukumwa, kwa sababu kuendelea kujazana kwenye viwanja, si tu kutaziathiri timu zitakazofungiwa kucheza mbele ya washangiliaji wao, bila kunawaweka kwenye 'afya' yenye mashaka mashabiki husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Mwapiza la nje hupata la ndani

**ANAYELAANI** au anayeapiza huko nje huishia kuipata laana ndani. Methali hii yaweza kutumiwa kwa mtu anayemtakia mwenzake mabaya kisha akapatwa na mabaya hayo hayo aliyomtakia mwenzake.

Si lazima yampate anayelaani au anayeapiza, bali yaweza kumpata mtoto wake au mjukuu na pengine hata kitukuu. Iwapo hivyo atasemaje?

'Utani' ni taratibu au desturi za kimila zinazowafanya watu wanaojuana waweze kuambiana au kutendeana jambo lolote la mzaha bila kuleta chuki au kero; maneno ya masihara; dhihaka. Tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana kweli na kuimarisha uhusiano wao.

Simba na Yanga zaitwa watani wa jadi. Mwaka 1935 zilikuwa moja lakini zikatengana mwaka uliofuatia – 1936 ilipoanzishwa Simba na kuzifanya ziwe mbalimbali. Mojawapo ilipofungwa mchezoni, nyingine ikawa ikiitania iliyofungwa.

Sasa mambo yamekuwa kinyume. Badala ya kutaniana, sasa wanachama na mashabiki wa timu hizo si watani tena bali wamekuwa maadui! Kinachofanya wawe maadui ni gozi la ng'ombe. Kwa lugha rahisi tuseme mchezo wa mpira wa miguu – kabumbu, kandanda, soka.

Hakuna mwanadamu anayezaliwa akiwa na akili ya kujichagulia umbile (namna kiumbe kinavyotarajiwa kuwa kulingana na jamii yake) apendalo. Hata wazazi hawawezi kuchagua jinsia ya mtoto wamtakaye kwani uumbaji hufanywa na Mwenyezi Mungu peke yake.

Miaka michache iliyopita, aliyekuwa msemaji wa Yanga ambaye sasa ndiye Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alikuwa rafiki mzuri wa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara.

Leo mtu wa Yanga kumsema vibaya mwenziye wa Simba kwa kutaja umbile lake si sahihi; ni ujinga. Huyo aliyetajwa kwa umbile alilo nalo, hakuchagua kuwa hivyo ila ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwani yeye ndiye muumba wa wote.

Je, huyo jamaa wa Yanga aliyesema maneno yale dhidi ya mwenzake wa Simba, ingekuwa yeye ndiye aliyeumbwa hivyo kisha mwenzake wa Simba akamwita kama alivyomwita mwenzie angefurahi? Hajui kuwa muumbaji ni Mungu aliyeumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo?

Heshima/hishima ni thamani ya utu wa mtu; adabu, staha. Heshimu ni kitendo cha mtu kuweka adabu kwa mwingine; stahi.

Ndo maana wahenga walisema "Heshima kitu cha bure" kwamba heshima hupatikana bila kununuliwa. Hii ni methali ya kutunasihi tuwe na heshima na adabu kwa wenzetu.

Jambo lingine linalokera ni jinsi Simba na Yanga zinavyosajili wachezaji kwa pupa huku zikionyeshana uwezo wa fedha kwa wachezaji wanaotaka kuwasajili. Itawezekanaje sehemu moja iwe na wachezaji zaidi ya watatu lakini bado wanasajiliwa wengine?

Msimu unaofuata anatolewa kwa mkopo kwenda timu ingine! Kwa nini alisajiliwa kama nafasi yake ina wachezaji wazuri zaidi yake? Naye kwa nini hakutambua hilo mapema ili asisajiliwe huko?

Timu zenye tamaa, fujo na kutaka kukomoana wakati wa usajili, kila mara huwa Simba na Yanga. Wachezaji hutaka kusajiliwa na vilabu hivyo kabla ya kujilinganisha na wenzao ambao wanaochezeshwa kila mechi.

Wachezaji wanatakiwa kujitathmini kabla ya kusaini kwenye timu hizo kongwe nchini badala ya kujipeleka kama vipofu wasioona waendako. Wajipime kama wanaweza kuchukua nafasi za wachezaji waliopo na kama viwango vyao viko chini watafute timu zingine.

Yasemwa "Tamaa mbele mauti nyuma." Maana yake ukiiweka tamaa mbele, mauti yatakuwa nyuma yakikufuata, mabaya yatakupata.

Hii ni methali ya kutumiwa kwa mtu mwenye tamaa nyingi. Huwafunza binadamu madhara yanayotokana na tamaa isiyokuwa na mipaka.

Mchezaji ajiulize: "Je, nikijisajili Simba au Yanga nitapata nafasi ya kucheza?" Akiona hatakuwa na nafasi hiyo, atafute kwingine atakapokuwa na nafasi hiyo. Vilabu navyo visisajili kwa kukomoana bali vifanye usajili wa dhati utakaowawezesha waliosajiliwa kucheza badala ya kuwa wachezaji wa akiba.

Katika yote hayo, wachezaji wanapaswa kuwatumia wanasheria wa chama chao watakaosoma kwa makini mikataba yao kabla ya kutia saini zao. Wanasheria watawasaidia kujua mazuri na mabaya yaliyoorodheshwa kwenye mikataba na kuwaelekeza kukubali au kukataa.

Ni muhimu wachezaji watambue umuhimu wao wanapocheza uwanjani kwani kuna uwezekano wa kuumia katika hali ya kawaida au hata kuvunjika mguu au mkono. Itokeapo hivyo, vilabu viwafanyie nini wachezaji hao?

Wakumbuke kuwa "Tamaa mbele mauti nyuma." Methali hii hutumiwa kwa mtu mwenye tamaa nyingi. Twafunzwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na tamaa isiyokuwa na mipaka.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# Kesi vigogo MSD sasa Julai 3

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepiga kalenda kesi inayowakabili vigogo wawili wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa zamani, Laurean Bwanakunu na mwenzake dhidi ya mashtaka matano ikiwamo kuratibu genge la uhalifu, kusababisha hasara na kutakatisha Sh. bilioni 1.6 mpaka Julai 3, mwaka huu.

Mbali na kuratibu genge la uhalifu, Bwanakunu anakabiliwa na shtaka la kutoa nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa MDS bila kibali cha Katibu Mkuu wa Utumishi.

Kesi hiyo imeahirishwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabati, baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa upelelezi wake bado haujakamilika.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Fatuma Waziri, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake bado haujakamilika.

Alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba tarehe ya kutajwa.

Hakimu Kabati alisema kesi hiyo itatajwa Julai 3, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mapema mahakamani hapo Wakili wa Serikali Faraja Ngukah, alimtaja mshtakiwa mwingine kuwa ni, Kaimu Mkurugenzi wa Logistiki wa MSD, Byekwaso Tabura na kuwasomea mashtaka yao.

Katika shtaka la kwanza ilidaiwa kuwa, kati ya Julai Mosi, 2016 na Juni 30, 2019 mahali tofauti jijini Dar es Salaam na nchini wakiwa watumishi wa umma waliratibu genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Upande wa Jamhuri ulidai shtaka la pili, kati ya Julai Mosi, 2016 na Juni 30, 2019 katika ofisi za MSD zilizopo Keko Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam washtakiwa kwa pamoja waliisababishia MSD hasara ya Sh. 3, 816,727,112.75.

Ngukah alidai katika shtaka la tatu, kati ya Julai Mosi, 2016 na Juni 30, 2019 ofisi za MDS, Bwanakunu alitumia madaraka yake vibaya kwa kuidhinisha nyongeza ya mishahara Sh. bilioni 3.8 kwa watumishi wa MSD bila kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Utumishi.

Katika shtaka la nne, tarehe za tukio, katika ofisi hizo, washtakiwa wote wawili wanadaiwa kushindwa kuhifadhi dawa na vifaa tiba na kusababisha kukosa ubora na hasara kwa MDS ya Sh. 85,199,879.65.

Shtaka la tano, tarehe za tukio katika ofisi hizo, washtakiwa walitakatisha Sh. 1,603,991,095.37 wakati wakijua ni zao la genge la uhalifu.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Ngukah alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika aliomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Upande wa utetezi ukiongozwa na mawakili Peter Kibatala, Kenedy Mgongolwa, Oscar Magotosa na Khalaghe Hashim, ulidai hauna pingamizi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Tamim Kambona (katikati), akifafanua jambo kwa wajumbe wa kamati ya siasa ya CCM ya wilaya hiyo, walipotembelea miradi ya maendeleo ya sekta ya afya iliyotekelezwa wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

# DC aagiza TAKUKURU kumhoji mtathmini

**Na Timoth Itembe, MARA**

MKUU wa Wilaya Tarime mkoani Mara, Mtemi Msafiri, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kumshikilia na kumhoji mtathmini wa kampuni ya White Knights, Dk. Medard Geho, baada ya kutilia mashaka tathmini ya fidia aliyosimamia katika kijiji cha Komarera.

Tathmini hiyo iliendeshwa kwa siku tatu kwenye eneo la kijiji hicho ambalo linatarajiwa kuchukuliwa na mgodi wa kuchimba madini ya dhahabu ulioko Nyamongo, Barrick ili kuitumia katika shughuli zake.

Akiongea jana mbele ya waandishi wa habari baada ya kutembelea maeneo ambayo yanatarajiwa kuchukuliwa na mgodi huo, mkuu huyo wa wilaya alisema mtathmini huyo amekuwa akihesabu mazao yaliyotegeshwa licha ya kuwa serikali imekataa kulipa fidia tegesha na kudai kuwa amekuwa akihesabu hata mazao yaliyopandwa na kutegeshwa juu ya mawe.

Kufuatia tuhuma hizo, mkuu huyo aliomba kazi hiyo ya kutathmini isimame kwa muda hadi hapo serikali itakapojiridhisha na kumtaka Mtathmini Mkuu wa Serikali kufika mahali hapo na kujionea hali halisi.

Msafiri alisema serikali kupitia Rais John Magufuli, ilishatangaza watu wote waliotegesha kwa lengo la kulipwa fidia hawatalipwa.

Alisema pia amesikitishwa na baadhi ya viongozi wa serikali kuwa mstari wa mbele kutegesha badala ya kuwa mfano kwa jamii ili kuwakataza na kuwazuia wale wote wenye nia mbaya.

Kadhalika aliwataka viongozi wanaohusika na kutegesha, kujisalimisha akiwamo Mwenyekiti wa Kijiji cha Komarera, Nyamaganya Marwa, ambaye amedai kutegesha nyumba na mazao.

Aliwataka wananchi wa Komarera na maeneo mengine ambayo yanatarajiwa kuchukuliwa na mgodi huo kuacha tabia ya kutegesha kwa kuwa kufanya hivyo ni kuihujumu serikali.

# TFS yaingia makubaliano upatikanaji miti

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umeingia makubaliano ya miaka mitatu ya upatikanaji wa malighafi ya miti, kutoa mitaji na kuwatafutia masoko ya mbao, wafanyabiashara wanaovuna misitu katika mashamba ya miti ya serikali.

Kamishna Mhifadhi wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo, alisema lengo la kuingia makubaliano hayo ni kuimarisha sekta ya misitu ili itoe mchango unaostahili kwa jamii na taifa.

"Ili tujenge nchi na hasa kupitia sekta ya misitu ni vyema kujadiliana na kukubaliana mambo kwa misingi ya uhifadhi. Tumeamua leo tuje na rasimu ya mkataba itakayokwenda kuwahakikishia wafanyabiashara upatikanaji wa malighafi kutoka kwenye mashamba ya miti ya serikali kwa miaka mitatu badala ya mwaka mmoja kama tulivyokuwa tunawapa mwanzoni," alisema Profesa Silayo.

"Hatutaishia kuwapa malighafi tu, tunaenda mbali zaidi kwa kuhakikisha wanakuwa na mitaji itakayowawezesha kuwekeza kwenye viwanda vya kisasa vya misitu. Katika ukuaji wa viwanda, masoko ya ndani na nje ni muhimu kwa juhudi binafsi au za serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade)."

Pia, Profesa Silayo aliwaongezea muda hadi Juni 30, mwaka huu, wavunaji waliolipia mgao wa miti kwenye mashamba ya miti ya serikali na kushindwa kumaliza kazi ya uvunaji ndani ya mwaka huu wa fedha kama mkataba unavyowataka kutokana na janga la corona.

Kwa upande wake Ofisa Biashara wa TanTrade, Gilbert Waigama, alisema mazao ya misitu hayana tatizo la masoko isipokuwa changamoto ipo kwa wadau wenyewe wa sekta hiyo kushindwa kufahamu namna ya kuyafikia.

Katibu wa Umoja wa Wavunaji Magogo SaoHill (UWASA), Dk. Basil Tweve, alisema kupitia mkataba huo mpya wa upatikanaji malighafi, utasaidia kwa kiwango kikubwa kukuza biashara ya sekta ya misitu nchini, kutokana na kuwa na sifa za kukopa kiwango kikubwa cha fedha tofauti na ilivyokuwa kipindi cha nyuma.

Alisema awali walikuwa hawana uhakika wa upatikanaji malighafi na hivyo ilikuwa inachangia wao kukosa sifa za kukopa mkopo mkubwa kwenye taasisi za fedha.

# Mkosamali atimkia CHADEMA

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa zamani wa Muhambwe, Felix Mkosamali, ametangaza kukihama chama cha NCCR-Mageuzi na kwenda CHADEMA ambako ametangaza nia ya kugombea ubunge kwenye jimbo hilo.

Mkosamali aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo mwaka 2010 hadi 2015, alitangaza uamuzi huo jana na kukabidhiwa kadi ya uanachama na Katibu wa CHADEMA, Ismaili Kangeta.

Katika ukurasa wa Twiter wa Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Mawasiliano na Itifaki, John Mrema, alimkaribisha Mkosamali kwa kuandika;

"Karibu CHADEMA ndugu Felix Mkosamali...umeona ukweli na kuamua kuhamia CHADEMA."

Naye, John Pambalu aliandika; "karibu sana kamanda Felix Mkosamali. Umekuwa mpambanaji mahiri katika kipindi chote cha maisha yako ya kisiasa. Sisi tunakukaribisha kwa moyo wa upendo na furaha, karibu tufanye kazi ya kuleta haki na usawa."

Kwenye mtandao huo waliandika kuwa mbunge huyo alikuwa miongoni mwa vijana machachari aliyeweza kujenga hoja bungeni.




Mchuuzi wa mihogo ya kukaanga akifanya biashara jirani na rundo la takataka katika eneo la Mabibo Sokoni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya yake na wateja wake. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Wakulima Tunduru wagoma kuuza ufuta

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAKULIMA wa ufuta wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamegoma kuuza zao hilo kutokana na bei ndogo iliyotolewa na wanunuzi.

Kutokana na hali hiyo wakulima hao wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuingilia kati kwa kuwatafutia wanunuzi watakaotoa bei nzuri.

Hayo yalijitokeza wakati wa mnada wa sita uliofanyika viwanja vya ofisi za Chama cha Ushirika cha Mlingoti Magharibi Amcos kwa kujitokeza wanunuzi wawili kwa bei ya Sh. 1,750.

Mwingine aliomba kununua kwa Sh. 1,730 ikiwa ni kabla ya makato ya kisheria.

Mbina Mnanka, Mohammed Salumu na Bakari Selemani wakizungumza na waandishi wa habari, walisema kwa mtazamo wa kawaida inaonyesha kuwa wanunuzi wanaojitokeza ni madalali ambao wamelenga kujinufaisha kupitia migongo ya wakulima.

Walisema wana imani na serikali katika utendaji wake na kwamba haiingi akilini katika mnada uliopita ufuta wao uuzwe kwa bei ya wastani wa Sh. 2,047.26 wiki moja baadaye bei ishuke kwa wastani wa Sh. 400.

Walisema bei hizo siyo rafiki kwa mkulima na hazizingatii gharama alizotumia wakati wa kuandaa shamba, kulima, kupalilia, kupulizia dawa na kuvuna.

"Bei zinazotolewa na madalali wa wanunuzi hao kwa kisingizio cha kushuka kwa bei za soko la dunia kutokana na corona, zinatukatisha tamaa wakulima kuendelea kulima zao hilo ikilinganishwa na gharama tunazotumia kuhudumia mazao yetu," alisisitiza Mnanka.

Wakulima hao pia walionyesha shaka kuwa huenda madalali hao wanafanya hivyo kutokana na kutokuwapo kwa ushindani wa kampuni zingine katika minada hiyo ambayo tangu ianze wanunuzi ni walewale.

Awali, mwakilishi wa Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakuliwa wilayani Tunduru (TAMCU), Imani Kalembo, Yasini Masiano, aliwataka wakulima walioshiriki mnada huo kuwa makini kusikiliza bei zinazosomwa kwenye barua za wanunuzi ili waweze kuchagua bei kubwa kuliko zote.

Akiahirisha mnada huo, Makamu Mwenyekiti wa TAMCU, Mussa Manjaule, alisema chama hicho kimeungana na uamuzi wa wakulima hao na kueleza kuwa mnada wa marudio utafanyika Juni 20, mwaka huu.

Alisema ingawa bei zinaendelea kushuka ikilinganishwa na bei za awali, iliyotolewa na wanunuzi hao siyo rafiki na haiwashawishi wakulima kuendeleza zao hilo kwa msimu ujao.

# Mabula afurahishwa NHC kukamilisha miradi

**Na Munir Shemweta, HAI**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kukamilisha ujenzi wa miradi ya jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Bomang'ombe na ofisi pamoja na nyumba za watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), zilizopo kwenye shamba la miti la Kilimanjaro Kaskazini, maarufu Rongai wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro.

Dk. Mabula alitoa pongezi hizo jana alipotembelea miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi na nyumba hizo akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na NHC na kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi kwenye mkoa huo.

Alisema, Shirika la Nyumba la Taifa kwa sasa linapaswa kupongezwa kutokana na juhudi kubwa inayofanya katika kutekeleza miradi yake ya ujenzi wa majengo ya ofisi na nyumba katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai na TFS kwa kujengwa katika viwango vinavyotakiwa.

Alisema, hivi sasa NHC imeaminiwa na serikali kwa kupatiwa miradi mbalimbali ya ujenzi ukiwamo wa majengo ya ofisi na nyumba za TFS nchini na hospitali za rufani za mikoa ya Mara na Mtwara.

"Tunapaswa kumshukuru Rais John Magufuli kwa kuamua kutoa fedha za ujenzi wa majengo ya ofisi na nyumba za wakala wa huduma za misitu kwenye mikoa mbalimbali, rais anataka watumishi wafanye kazi katika mazingira mazuri," alisema Dk. Mabula.

Alisema NHC inapaswa kuhakikisha miradi yote inayokabidhiwa inakamilika kwa wakati na ujenzi unaokidhi viwango na ubora unaotakiwa ili kujenga imani kwa wananchi na serikali.

Akielezea utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi na nyumba za watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Meneja wa NHC, Mkoa wa Kilimanjaro, Juma Kiaramba, alisema mradi huo ambao mpaka sasa umetumia Sh. 639,494,580.18, ulianza Septemba mwaka jana na tayari kazi za ndani kwa majengo yote manne umekamilika kwa asilimia 100 na kusisitiza kuwa shirika lake linatarajia kukamilisha zilizobaki za nje katika kipindi cha muda mfupi.

Kaimu Meneja wa TFS Kilimanjaro Kaskazini, Joel Naasi, alimweleza Naibu Waziri Mabula kuwa kupitia shamba la miti la Kilimanjaro Kaskazini Wakala umefanikiwa kukusanya maduhuli ya Sh. 3,688,849,489.68 hadi kufikia Mei, mwaka huu wa fedha.

Akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi wa ofisi ya ardhi Mkoa wa Arusha na halmashauri za mkoa huo, Dk. Mabula, alisema uamuzi wa kuanzisha ofisi za ardhi za mikoa ni kutaka kuondoa kero za ardhi na kusogeza huduma za sekta hiyo karibu na wananchi.

# Wakulima kuhamasishwa kilimo cha mkonge

**Na Augusta Njoji, KONGWA**

BODI ya Mkonge nchini imeanza kuhamasisha kilimo cha zao hilo katika maeneo mbalimbali nchini ili kuzalishwa kwa wingi ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Hatua hiyo imekuja wiki mbili baada ya Waziri Mkuu kuagiza bodi hiyo kuhakikisha inaongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 36,000 za sasa hadi kufikia tani 120,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2025.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Saddy Kambona, alipokuwa akihamasisha kilimo hicho katika Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

Alisema mkakati wa kulifufua zao hilo umeanza na utakuwa endelevu kwa wilaya na mikoa mingine nchini.

"Bodi ya Mkonge ilikuwapo tangu mwaka 2000 awali ilikuwa Mamlaka ya Mkonge Tanzania, miaka ya hivi karibuni uzalishaji ulishuka kwa kiasi kikubwa, lakini kwa sasa uzalishaji umefikia 36,000 kwa mwaka," alisema.

Alieleza kutokana na agizo hilo la Waziri Mkuu wameanza kuhamasisha wakulima wadogo ili kujikita kwenye kilimo hicho.

"Tumempata mkulima mmoja ambaye tayari amelima hekari 40 za mkonge na tumekuja kumtembelea hapa Kongwa ikiwa ni sehemu ya kuendelea kuhamasisha wakulima wengine," alisema.

Naye Mkuu wa Idara ya Mipango, Masoko na Utafiti, Hassan Kibarua, alisema zao hilo linatoa mwanya kwa mkulima kulima zaidi ya zao moja kwenye shamba moja na kumpa faida zaidi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, alisema wilaya hiyo itakuwa ya mfano katika kilimo cha mkonge pindi watu wake watakapopata elimu ya kutosha.

"Unapohamasisha wananchi unawafanya wananchi kulima kilimo cha kiuchumi kama tulivyofanya kwenye kilimo cha korosho, na mategemeo yetu itaongeza kipato cha mtu mmoja mmoja kwa wananchi," alisema.

# Serikali kuwaendeleza wabunifu kibiashara

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imetenga Sh. milioni 750 kwa ajili ya kuwaendeleza washindi 70 wa mashindano ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu (MAKISATU) ili kufanya ubunifu wao kuwa wa kibiashara.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini hapa, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako, alipokuwa akitangaza washindi wa mashindano hayo kwa mwaka 2020.

Alisema fedha hizo zitatumika kuwaendeleza wabunifu hao ili kazi zao ziwe kibiashara na kuwainua kiuchumi.

Pia alisema serikali itaendelea kutenga fedha zaidi mwaka hadi mwaka kwa ajili ya kuendeleza ubunifu nchini.

"Natoa rai kwenu na washindi wote kuendeleza bunifu zenu ili kuhakikisha zinakuwa fursa za kiuchumi kwenu," alisema Prof. Ndalichako.

Kadhali alisema serikali imetoa shilingi milioni tano kwa washindi wa kwanza kwa makundi yote, Shilingi milioni tatu kwa washindi wa pili na Shilingi milioni mbili kwa washindi wa tatu.

"Makundi yaliyoshiriki katika mshindano haya ni pamoja na shule za msingi, sekondari, vyuo vya ufundi stadi, vyuo vya ufundi wa kati, vyuo vikuu, taasisi za utafiti na maendeleo pamoja na mfumo usio rasmi," alisema.

Alisema mashindano hayo hufanyika kila mwaka na kutoa fursa kwa wabunifu kujitangaza kwa wadau na watumiaji wa ubunifu na teknolojia zao.

"Mshindano yaliyopita tulianzia sekondari baadaye tulifanya tathmini na kubaini tunakosa kuibua vipaji vya watoto wadogo ndio maana tukaanzia kwenye shule za msingi na makundi mengine hadi vyuo vikuu," alisema.

Vile vile, alisema kumekuwapo na ongezeko la washiriki na kwa mwaka huu walishiriki wabunifu 651 ikilinganishwa na mwaka 2019 walikuwa 415.



Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Magembe Makoye, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, wakati akitoa taarifa ya kufanya uchaguzi mkuu wa kitaifa mwaka wa chama hicho, utakaofanyika Julai 16 mwaka huu, jijini humo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Skimu umwagiliaji zaidi 170 zajengwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUMLA ya skimu za umwagiliaji 179 zimejengwa na kukarabatiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) kwa kipindi cha miaka mitano na hivyo kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Daudi Kaali, alipokua akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya umwagiliaji kwa miaka mitano.

Alisema kutokana na ukarabati na ujenzi huo kumeongeza eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 461,000 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 50.7.

Mkurugenzi huyo alisema pia mradi wa kuendeleza wakulima wadogo (SSIDP), ambao ulitekelezwa katika awamu tatu kwenye mikoa na wilaya mbalimbali nchini kumechangia mafanikio hayo.

"Awamu ya kwanza utekelezaji wa mradi huu uligharimu Sh. bilioni 15.37 na ulihusisha ujenzi na ukarabati wa skimu 48 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 13,722," alisema.

Alisema awamu ya pili ilihusisha skimu 61 zenye ukubwa wa hekta 22,312 uliogharimu Sh. bilioni 20.1.

"Awamu ya tatu ya utekelezaji ilihusisha skimu 16 na kati ya hizo tisa zimekamilika na awamu hii inategemea kugharimu Sh. bilioni 6.3 na hekta 1090 zinategemewa kuongezeka," alisema.

Kwa upande wake, Mhandisi Daniel Manase kutoka kitengo cha ukaguzi na udhibiti ubora wa miradi ya umwagiliaji wa NIRC, alisema mafanikio hayo yamechangia uzalishaji wa zao la mpunga kuongezeka kutoka wastani wa tani 1.8- 2.0 kwa hekta hadi tani 4.0-5.0.

Alisema kwa zao la mahindi uzalishaji umeongezeka kutoka tani 1.5 hadi 3.7-5.0 kwa hekta, vitunguu pia uzalishaji umeongezeka kutoka tani 13 hadi 26 kwa hekta na nyanya kutoka tani tano hadi 18 kwa hekta na hivyo sekta ya umwagiliaji kuchangia asilimia 24 ya mahitaji yote ya chakula nchini.

Akizungumzia mikakati ya Tume kwa miaka mitano ijayo, Kaimu Mkurugenzi wa Usanifu na Utafiti wa Tume hiyo, Gregory Chigwie, alisema imejipanga kutekeleza miradi ya kimkakati kwa kujenga miundombinu mbalimbali ya umwagiliaji kwenye baadhi ya mabonde ya mito nchini.

Alisema wanatarajia kukusanya Sh. milioni 300.4 kwa kipindi hicho kupitia vyanzo mbalimbali katika Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji.

HABARI ZANZIBAR

# Makamu M/kiti TADEA atangaza nia urais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI asiye na Wizara Maalumu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ada TADEA, Juma Ali Khatib, ametangaza nia ya kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar kama chama chake kitampa ridhaa ya kugombea nafasi hiyo.

Khatib alitangaza dhamira hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi huku akiwaaga wajumbe wenzake kufuatia kumalizika muda wa baraza hilo ambalo linatazamiwa kuvunjwa rasmi na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein leo.

Alisema akiwa waziri na mwakilishi wa kuteuliwa na Rais Ali Mohamed Shein alipata uzoefu mkubwa wa kiutendaji ikiwamo kujenga tabia ya uvumilivu na kufanya siasa za kistaarabu.

"Mheshimiwa Spika mimi Juma Ali Khatib, natangaza kutia nia kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Ada TADEA kama kitanipa ridhaa ya kupeperusha bendera hiyo," alisema.

Khatib alimshukuru Dk. Shein kwa kumteua kuingia katika serikali na kuunda Baraza la Mapinduzi licha ya kuwa anatoka katika chama cha upinzani, kitendo alichosema kinachoonyesha uaminifu wa hali ya juu.

Alisema amejifunza mambo mengi, lakini kubwa ni uadilifu, uvumilivu na kuweka mbele uzalendo wa kuwatumia wananchi.

"Sasa nimeiva kisiasa katika kipindi ambacho nimefanya kazi na Rais Ali Mohamed Shein... uongozi misingi yake mikubwa ni uadilifu, uaminifu na kuweka mbele uzalendo wa kuwatumia wananchi," alisema.

Alisema kuwa mwaminifu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulingana na kiapo chake alichokula na kuahidi daima kamwe kutokwenda kinyume na serikali iliyopo madarakani.

"Hata nisiporudi serikalini...kiapo changu nilichokula cha kuwa mtiifu na mwadilifu kwa serikali iliyopo madarakani nitaendelea kukiheshimu katika muda wote wa maisha yangu," alisema.

# ZJMC yapandishwa hadhi kuwa chuo kikuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHUO cha Uandishi wa Habari cha Zanzibar (ZJMC), kimehamishwa na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), lengo likiwa kuongeza ufanisi wa taaluma ya mawasiliano ya habari kwa umma kuwa bora.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba SUZA kimejipanga kukipokea chuo cha uandishi wa habari kuwa sehemu ya chuo kikuu katika taaluma ya habari na mawasiliano ya umma.

Alisema maandalizi yote yamekamilika na kuwatoa wasiwasi baadhi ya wajumbe waliochangia mswada huo ulioletwa kwa hati ya dharura kwamba SUZA hakina maandalizi kwa ajili ya kupokea baadhi ya taasisi za elimu kuwa sehemu ya chuo hicho.

"Mheshimiwa Spika maandalizi yote yamekamilika ya kukipokea Chuo cha Uandishi wa Habari kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA)...Wajumbe na wanafunzi wote msiwe na wasiwasi," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia mswada huo walikuwa na wasiwasi kuhusu uwezo wa SUZA kupokea taasisi mbalimbali za elimu zilizounganishwa kikiwamo Chuo cha Uandishi wa Habari.

Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, Dk. Mwinyihaji Makame, alisema zipo baadhi ya taasisi za elimu zilizounganishwa na SUZA zinasuasua katika utendaji huku walimu na baadhi ya watumishi wakipata tatizo la fedha na mishahara.

"Mheshimiwa Spika mimi bado napata wasiwasi mkubwa kuhusu uamuzi wa kukiunganisha Chuo cha Uandishi wa Habari na kukipeleka sehemu ya chuo kikuu cha (SUZA)...Tatizo zipo taasisi za elimu ambazo zimeunganishwa na SUZA bado utendaji wake unasuasua," alisema.

Naye Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, alisema lengo la kukipeleka chuo hicho na kukifanya sehemu ya chuo kikuu ni kuboresha taaluma hiyo kwa kuipandisha hadhi, huku wahitimu wake wakitambuliwa kuwa sehemu ya chuo kikuu.

Alisema kwa muda mrefu kuna tatizo la uhaba wa walimu wenye sifa na kwa kukifanya kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa, matarajio ni kuwapo kwa ufanisi wa hali ya juu na ubora wa taaluma inayotolewa kwa wahitimu.

"Hayo ndiyo matarajio yetu kuona kwamba ubora wa elimu na wahitimu wanaohitimu katika chuo hicho wanakuwa na sifa na kutambuliwa sehemu yoyote... wajumbe msiwe na wasiwasi serikali imejipanga kabla ya suala hili kulifikisha hatua hiyo," alisema.



Waziri asiye na Wizara Maalum, Juma Ali Khatib (katikati), akizungumza na Ofisa Habari wa Baraza la Wawakilishi, Himidi Choko (kushoto) na Waziri asiye na Wizara Maalum, Said Soud, nje ya ukumbi wa baraza hilo, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Balozi Iddi aaga siasa, asema atakayemrithi Shein kazi ndogo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais na Kiongozi Mkuu wa shughuli za serikali katika Baraza la Wawakilishi, Balozi Seif Ali Iddi, amesema rais mtarajiwa ana kazi ndogo ya kukamilisha mambo ya msingi ikiwamo miradi ya kimkakati ambayo tayari imo katika bajeti ya utekelezaji.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo wakati akiwaaga wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwaambia ana achana na siasa kutokana na umri.

Alisema serikali inayomaliza muda wake ya Dk. Ali Mohamed Shein, imefanya mambo makubwa na mengi ikiwamo kutekeleza miradi muhimu ya kimkakati ambayo baadhi yake imekamilika na mengine inahitaji utekelezaji.

Alisema mradi wa jengo la maegesho ya ndege pamoja na abiria la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, unaendelea vizuri na umefikia hatua ya asilimia 72 kwa kutumia fedha za ndani za makusanyo ya kodi.

"Mradi huu ni muhimu, utekelezaji wake ulisuasua kwa hatua tofauti...hivi sasa tunaendelea kuukamilisha kwa kutumia fedha za ndani zinazotokana na makusanyo ya kodi," alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka kumi, serikali imefanikiwa kujenga majengo ya ofisi zake na kuondokana na yasiyo na hadhi katika Mji Mkongwe.

"Katika kipindi cha miaka kumi tumejenga ofisi nyingi za serikali zenye hadhi kwa kutumia fedha za ndani za makusanyo ya kodi," alisema.

Alisema rais anayekuja na serikali yake atatakiwa kufuata nyayo za Rais Shein na kuangalia miradi iliyopo ambayo inatakiwa kukamilishwa katika hatua za mwisho.

Balozi Iddi alisema kutokana na umri kuwa mkubwa, anastaafu katika siasa na hatogombea nafasi yoyote na kuwaachia vijana wengine kusukuma gurudumu la taifa la maendeleo.

Aliwapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano akiwamo Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, mawaziri na manaibu kwa ushirikiano uliomwezesha kutekeleza majukumu yake na kuwatumikia wananchi kwa uaminifu mkubwa.

"Mimi sasa nastaafu siasa, nawapongeza viongozi wote wa Baraza la Wawakilishi ukiwamo wewe Spika pamoja na wapigakura wa jimbo langu la Mahonda kwa ushirikiano mkubwa ambao umeniwezesha kuitumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika nafasi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa miaka kumi mfululizo," alisema.



MAJINA TUZO ZA BET HADHARANI UK. 14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# HARMONIZE KALIANZISHA

## Usukaji nywele, kuvaa herini Mungu wake anajua

MKALI wa Bongo Fleva, Harmonize, amesema Mungu anamwongoza kwa kila jambo, hata usukaji wa nywele, kuvaa herini na kuchora tattoo inatokana na mapenzi yake.

Akizungumza na EATV, mwimbaji huyo wa Albam ya 'Afro East' amesema kutokana na yeye kumweka mbele Mungu, anaamini kila anachokifanya kinatokana na uwezo wake.

Kauli yake hiyo ambayo imeibua mjadala mitandaoni, inaonekana kwenda kinyume na imani yake ya dini na kwamba baadhi ya mashabiki wake wamehoji uhalali wa kumshirikisha Mungu katika masuala hayo.

"Kila unachokifanya kwenye maisha tambua kwamba Mungu anakupa mwongozo, hata kipaji nilichonacho yeye ndiye amenipa, siwezi kujutia kufanya vitu ambavyo vitanifanya nionekane kama msanii, kama kusuka nywele, kuchora tattoo au kuvaa herini kwa kuwa namuheshimu na nikipata nafasi nasali".

Hata hivyo, katika mahojiano hayo Harmonize, amesikika akiomba radhi kama atakuwa amekwenda kinyume na kwamba yeye anazungumzia kile ambacho anakielewa katika upeo wake wa kuelewa.

Akizungumzia mtindo wake wa kusuka nywele, Harmonize, amesema ana mpango wa kurudia kwani ndio umemtambulisha duniani kama mwanamuziki mahiri kutoka Afrika Mashariki.

"Ule mtindo nilijaribu kufanya kitu cha tofauti, nasikitika nilizitoa kwa sababu ya mwezi wa Ramadhan na mimi ni Muislam nafunga, nikaona nizitoe, lakini nilikuwa nazipenda na natamani nirudi kwenye style ile kwa sababu, inanifanya nionekane wa tofauti, " amesema Harmonize. "

BASI SAWA

## BASATA inapojipanga kufungua burudani

BARAZA la Sanaa Tanzania (BASATA), limemshukuru Rais Magufuli, kwa kurejesha shughuli za kisanaa kama ilivyokuwa awali, baada ya kuzuiliwa kwa muda kutokana na janga la corona.

Akithibitisha hilo kwenye kipindi cha Planet Bongo ya East Africa Radio, Katibu Mtendaji wa BASATA, Godfrey Mngereza, amesema tayari amekaa na wadau wote wa sanaa ili kujadili jinsi gani watafanya baada ya kufunguliwa kwa burudani.

"Tayari tulikuwa tumekaa vikao na wadau wote wa sanaa siku ya Mei 28, ili kuangalia ni namna gani ambavyo tunaweza kufanya kazi zetu huku tunaishi na corona, tulichukua yale maoni na tukapeleka wizarani, ndiyo maana Rais mwenyewe alitoa tamko ili kurejesha shughuli za michezo, sanaa na burudani, na sisi kama BASATA tumetoa ruksa, lakini haina maana wasanii wavunje sheria na kanuni" amesema Mngereza.



## Chidi Benz kama 'handsome boy' Bongo Fleva

MSANII mkongwe wa Hip-hop, Chidi Benz, amesema mwonekano wake wa sasa amezidi kuwa 'handsome' kupita wasanii wote wa muziki huo nchini.

"Tangu nimeanza kufanya vitu vyangu mwenyewe naona vinaenda, vinatokea na vinakua, napata msaada kwa watu kadhaa na wanasifia naishukuru East Africa kwa sababu vyombo vingine vinanisikilizia, lakini wao hawajawahi kuwa hivyo, heshima kwa dada yetu Regina."

Kuhusu upande wa mwonekano wake wa sasa Chidi Benz amesema, hakuna msanii wa Hip-hop "handsome boy" kama yeye kwa sababu anavutia kwa kinadada.





## NELSON: Morani anayetamba muziki wa injili

NELSON Nagunwa (28) ni kijana kutoka jamii ya Kimasai, ameamua kuacha ufugaji na sasa amejikita katika muziki wa injili.

Nagunwa, tayari ametoa singo yake ya kwanza inayoitwa 'Kwa Yesu Kuna Raha' ambayo inafanya vizuri katika mitandao ya kijamii na vituo mbalimbali vya radio na runinga.

Akizungumza na BT, Nagunwa amesema wimbo huo ni mwanzo wa safari yake ya kutoa huduma kwa Mungu kwa kupitia muziki na kwamba nyimbo zingine ziko mbioni.

"Nilikuwa na wito wa kumtumikia Mungu tangu nikiwa mtoto, hii inatokana na familia yangu kuwa watu wa dini sana, naamini kupitia wimbo huu "Kwa Yesu Kuna Raha' watu wataweza kubadilika na kuwa wanyenyekevu," amesema Nagunwa.

Amesema kwa sasa yupo chini ya meneja wake Allen Chusunga, ambaye anamiliki studio ya Holy Production.

"Kupitia meneja wangu nimeanza kuona ndoto yangu inatimia, nyimbo zangu zinarekodiwa na kuzimamiwa na Holy Production jambo ambalo nafarijika," ameongeza kusema.

Nagunwa, amekuwa na matarajio ya kuwa staa katika muziki wa injili, na anatamani kuwa na mafanikio kama walivyo wasanii wakubwa kama Enock Jonas na Matha Mwaipaja.



## Ndaro atangaza kugombea ubunge Musoma Vijijini

MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Basogo Nashon Ndaro, maarufu kama 'Model' ametangaza nia ya kugombea Jimbo la Musoma Vijijini ambalo kwa sasa mbunge wake ni Profesa Sospeter Muhongo.

Akizungumza na BT, Ndaro amesema lengo la kutaka kugombea ubunge wa jimbo hilo ni kutaka kuongeza kasi ya maendeleo ambayo yapo nyuma kwa muda mrefu.

"Jimbo la Musoma Vijijini kwa muda mrefu limekosa maendeleo, kila mbunge anayeingia hakidhi matarajio ya watu wa Musoma Vijijini. Mimi kama kijana ninaamini nitaweza kusukuma nguvu mpya katika utendaji wa kazi," amesema Ndaro.

Aidha, amesema hana wasiwasi kukabiliana na Profesa Muhongo, akiamini wananchi wa jimbo hilo na Wanaccm, wanajua wapi walipo na vipi watafikia ndoto zao.



## Wanamuziki watano wenye sauti ya zege

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE uimbaji kuna sauti za juu, za kati na zile za chini. Ukitaka uzifaidi sauti hizi vizuri basi upate waimbaji ambao wanaimba kwa staili ya kwaya.

Kwenye muziki wa dansi pia kuna utamu unaopatikana kutokana na waimbaji kuimba kwa kuitikia, kupokezana na kuimbisha mmoja mmoja.

Hii inafanya ladha ya aina yake kwenye muziki ambapo hupatikana ladha ya waimbaji wenye sauti za juu, za kati na hata zile za chini ambazo wataalamu wanaziita 'deep voice'.

Mara nyingi mashabiki wengi wa muziki huvutiwa zaidi na wanamuziki wenye sauti nyororo za juu. Lakini wapo wachache ambao huvutiwa na wanamuziki wenye sauti nzito na hasa wanapoimbisha au kuimba peke yao.

Leo tunawaletea wanamuziki wa dansi ambao wana sauti nzito zilizovutia mashabiki wengi nchini Tanzania.

**HEMED MANETI**

Alikuwa ni mwimbaji na kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz. Ni mmoja ya wanamuziki wenye sauti nzito ambayo aliitumia vema na kuondokea kupendwa na kujizoela mashabiki wengi nchini.

Maneti ambaye alifariki Mei 31, 1990, jijini Dar es Salaam, alitunga na kuimba nyimbo mbalimbali ambazo zilimpatia umaarufu mkubwa.

Ukitaka uisikie vema sauti yake, tafuta zile ambazo aliimba peke yake baadhi ya vipande kama 'Vicky', 'Masido', 'Tabu', 'Mundinde', 'Mary Maria', na nyingine nyingi ambazo zilimfanya kuwa staa Afrika Mashariki.

**JERRY NASHON 'DUDUMIZI'**

Huyu aliitwa 'Dudumizi' kutokana na aina yake ya uimbaji ambapo sauti yake inafanana na ndege huyo, kutokana na staili yake ya kuitetemesha sauti yake nzito.

Ni mwimbaji na mtunzi aliyepitia bendi nyingi kama Magereza Jazz, Vijana Jazz, Bima Lee na nyinginezo.

Anatajwa kuwa ndiye mwimbaji mwenye sauti nzito zaidi kuliko wengine wote nchini Tanzania.

Nyimbo ambazo zimemtangaza sana na kujipatia mashabiki wengi ni 'Makulata', 'Baba Shani', 'Pendo', 'Pesa Zanisumbua' ambazo vipande virefu aliimba peke yake na kucheza vema na sauti yake nzito. Alifariki mwaka 1995 jijini Dar es Salaam.

**MUHIDINI GURUMO**

Ni mwimbaji nguli na mkongwe nchini Tanzania tangu miaka ya 60. Alifariki dunia 2014 na kuacha simanzi kwenye tasnia ya muziki nchini, akiimba miaka mingi zaidi kuliko mwanamuziki yoyote yule.

Huyu naye ni mmoja wa wanamuziki waliokuwa na sauti nzito zilizokuwa zikirindima kwenye redio nchini.

Ana nyimbo nyingi sana, lakini baadhi alizoziimba baadhi ya vipande peke yake ni 'Chatu Mkali', 'Rabana', 'Mv Mapenzi namba moja', 'Isihaka' na nyingine nyingi.

**ADAM BAKARI**

Huyu alipewa jina la utani 'Sauti ya Zege' kutokana na kuwa na sauti nzito. Marehemu Adam Bakari alikuwa mwimbaji na mtunzi ambaye alipitia bendi nyingi na kuwa mmoja wa wanamuziki wanaoongoza kwa kuhama.

Ndiye mtunzi wa nyimbo maarufu ambazo naye aliziimba kama 'Ogopa Tapeli', 'Azam Umeniumbua' za Vijana Jazz, pia 'Nachelewa Stendi ya Basi' wa Tomatoma.

**MABROUK MOHAMED**

Hakupata jina kubwa sana, lakini ukizisikiliza nyimbo za Mwenge Jazz Band utasikia sauti nzito ya Mabrouk Mohamed na kuwa ni mmoja wa wanamuziki wenye sauti za zege. Wakati wa mwishoni mwa uhai wake alipitia bendi ya TOT baada ya kustaafu Jeshi la Wananchi na huko ndiko umauti ulipomfika.

## Mume Aliyekimbia; Baba anayekula kuku na mayai yake

**Na Adam Fungamwango**

NI tabia iliyojengeka kwa baadhi ya wanaume, kuwapa ujauzito wasichana na kisha kuwakimbia.

Iwe mjini au vijijini, wanaume wengi wamekuwa na tabia hiyo, ambayo mbali na kuwa inawaharibia maisha watoto wa kike, lakini hata wao wenyewe inakuja kuwadhuru na kuwaaibisha.

Leo tutaiangalia filamu ya 'Mume Aliyekimbia', ambayo inaelezea kisa cha kusikitisha kilichotokana na kosa la mtu mmoja ambaye anakuja kufanya kosa lingine kwa mara ya pili linaloleta matatizo kwenye familia yake na yeye mwenyewe.

Imechezwa na Suleiman Barafu, Stanley Msungu, Riyama Ally, Najma Ally na Catty Rupia na wengineo. Inaanza kuonyesha kuwa Barafu anaishi vema na mkewe Catty.

Shetani anamwingia na kuingia kwenye penzi na msichana mwanafunzi wa sekondari aitwaye Najma. Penzi linanoga kiasi cha mkewe kujua kuwa mumewe ana matatizo kwa sababu alibadilika tabia.

Riyama ambaye ni mama wa Najma kutokana na kuletewa pesa na binti yake akawa hajui binti yake aendelee na masomo au aendelee na mchezo wake mchafu.

Chovya chovya humaliza buyu la asali, Najma anapata mimba. Hii ilimchanganya mama yake, pamoja na Barafu mwenyewe.

Najma kuitoa hataki na Barafu ana mke, lakini alimficha Najma. Binti anajiona bora azae ili awe mke wa Barafu.

Barafu anaandaa mbinu kabambe na rafiki yake Msungu. Mbinu yenyewe ni kumuua Najma na si vinginevyo. Kwa sababu amekataa kutoa mimba na yeye ni mwanafunzi kitu ambacho kilimtisha Barafu kuwa anakaribia kuingia kwenye mdomo wa jela.

Msungu anamuua Najma, lakini anakamatwa alipokuwa anakwenda kutupa maiti iliyokuwa ndani ya gari.

Hata hivyo anasema kuwa yeye si mhusika ila alitumwa. Anaachiwa kwa sharti moja tu la kumkamatisha mhusika.

Barafu katika pitapita yake anakutana laivu na Riyama, mama yake marehemu Najma. Wanakumbukana. Miaka mingi iliyopita kwenye kijiji kimoja Tanzania, Barafu alimpachika mimba Riyama na kukimbia. Alijifungua mtoto wa kike akamwita Najma. Kumbe Barafu alimpa mimba binti yake. Lakini alifanya njama ya kumuua.

Polisi na Msungu wanakwenda kumchukua Riyama, wakimweleza kuwa wamempata muuaji wa binti yake. Wanakwenda nyumbani kwa Barafu na kumkamata. Riyama alipoona sura ya Barafu na kujua kuwa yule ndiye alimpa mimba binti yake na pia kumuua anaanguka chini na kuzirai.

Tayari alitambua kuwa yule ndiye mzazi mwenzake na ndiye aliyempa ujauzito binti yake na kumuua.



# 'Blood and Water' yapagawisha mitandaoni

MTANDAO wa Netflix, umetambulisha filamu mpya ya Kiafrika, inayoitwa 'Blood and Water' katika msimu wake wa pili.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Netflix ilitaja filamu hiyo ambayo imechezwa na wasanii wa Afrika Kusini, ni moto wa kuotea mbali kutokana na kujaa fitina, vurugu, furaha na mapenzi.

Mastaa waliomo kwenye 'Blood and Water' ni Ama Qamata, ambaye anafahamika kama Puleng Khumalo, Natasha Thahane, Thabang Molaba, Gail Mabalene, Sello Maake ka Ncube, Xolile Tshabalala na Cindy Mahlangu.





## Perry kuchangisha fedha

MWIGIZAJI kutoka Hollywood, Tyler Perry, ameanza mchakato wa kuwasomesha watoto wanne walioachwa na Rayshard Brooks, ambaye aliuawa hivi karibuni na polisi wa kizungu.

Rayshard ambaye ni Mmarekani mweusi alipigwa risasi na ofisa wa polisi wa Jimbo la Atlanta nchini Marekani Juni 12, wakati alipokamatwa akituhumiwa kutumia dawa za kulevya.

Kulingana na jarida la PEOPLE, Perry amesema familia ya Brook, inahitaji msaada kwa sasa.


"Moyo wake umekwenda mbali na familia tangu kutokea kwa kisa hiki, lakini kuna umuhimu wa kuwasaidia watoto wake," amesema Perry.

## Majina tuzo za BET hadharani

KITUO cha burudani cha televisheni cha Black (BET), kimetangaza majina ya wasanii watakaowania tuzo za mwaka huu.

Katika majina yaliyotajwa, ya wasanii wa Nigeria ni, Burna Boy na Mavin Rema, yamejitokeza.

Wanamuziki wengine wa Afrika, ambao majina yao yamewekwa hadharani ni rapa kutoka Afrika Kusini, Sho Madjozi na Innos'B kutoka nchini DRC.





## Chioma yakikuzidi utasema

CHIOMA ambaye ni mchumba wa mwanamuziki wa Nigeria, Davido, amekuja juu baada ya kusambaa kwa uvumi kwamba anapata manyanyaso ya kijinsia ndani ya nyumba.

Katika ujumbe aliposti kwenye ukurasa wake wa Instagram, Chioma amewaambia mashabiki wake kwamba hajakabiliana na jambo lolote la unyanyasaji kutoka kwa Davido.

"Najua watu wangu kwamba mapenzi huwa yanakabiliwa na kila aina ya uvumi, ukweli hakuna manyanyaso kati yangu na Davido," ameandika Chioma.

## Dbanj pole yako, yote yataisha

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Dapo Oyebanjo, maarufu kama Dbanj, hatimaye amejitokeza na kukanusha madai ya ubakaji yaliyotolewa dhidi yake na mwanamke mmoja.

Wiki iliyopita, mwanasoka Benjamin Ese, alidai kwamba Dbanj alimbaka rafiki yake mwaka 2018, katika hoteli ya Glee huko Kisiwa cha Victoria, jijini Lagos.

Katika ujumbe aliouweka katika ukurasa wake wa Instagram,msanii huyo alikana tuhuma huzo akisema ni uwongo uliopitiliza.

"Leo itakuwa wakati pekee nitasema kuhusu tuhuma za uwongo kutoka shimo la kuzimu. Nimechagua kufanya hivyo kwa sababu tukio hilo ni pigo kwa ndoa yangu na mke wangu mrembo, familia yangu yote, na wale wanaoniamini," aliandika.



# SABABU TANO MUHIMU ZA KUSAJILI NEMBO BIASHARA

**Na Mwandishi Wetu**

ALAMA ya biashara au huduma ambayo kwa wengi hujulikana kama nembo au 'logo' ni alama ya kipekee ambayo inatambulisha aina fulani ya bidhaa au huduma inayotolewa au kuzalishwa na mtu, kikundi au kampuni fulani.

Katika historia, usajili wa alama hizi ulianza kufanyika chini ya sheria katika karne ya 19 ingawa ni bayana kwamba hata kabla ya hapo alama hizi zilikua zikitumika.

Moja ya sababu kubwa iliyosababisha kuanza kusajili alama za biashara au huduma ni ukuaji wa teknolojia hasa kuongezeka kwa masafa ya vyombo vya habari na kuwafikia watu wengi zaidi.

Katika historia alama za mwanzo kabisa kusajiliwa ni pamoja na 'Deviled Entremets' ambayo ilisajiliwa Mwaka 1870 na Kampuni ya William Underwood huko Boston, Marekani.

Mwaka 1875, Mfanyabiashara William Bass aliingia katika historia ya kusajili Alama ya Biashara ya kwanza nchini Uingereza iliyojulikana kama 'Red Bass triangle'.

Alama hii ilikua na mwonekano wa pembe tatu nyekundu (kitako kikiwa chini na ncha kali ikiangalia juu) na maneno yaliyosomeka Bass.

Nchini China alama ya kwanza kusajiliwa ilijulikana kama 'Nestle Eagle Brand' ambayo ilisajiliwa mwaka 1874. Hizo ni baadhi ya alama za kwanza kusajiliwa katika nchi mbalimbali.

Kwa Tanzania alama ya biashara ya kwanza kusajili ilijulikana kama 'His maters Voice' iliyosajiliwa Septemba 11, 1922.

Kila jambo linalofanyika kuna sababu kadhaa nyuma yake, vivyo hivyo kwa usajili wa alama hizi. Makala hii itaangazia sababu tano kuu za kwanini ni muhimu kusajili alama za biashara au huduma "nembo".

**UTAMBUZI WA BIDHAA/HUDUMA**

Sifa kuu ya alama ya biashara au huduma ni kutofautisha bidhaa moja kati ya nyingine zinazofanania, mfano bidhaa ya maji ya chupa ya kunywa zote ni bidhaa ila zinatofautishwa na alama ya bidhaa nembo.

Kwa bidhaa za aina moja zingiapo sokoni ni vigumu sana kutambua utofauti wake, hivyo kumfanya mnunuzi kushindwa kuwa na uhakika na bidhaa atakayonunua.

Hii inaweza kumfanya mteja kushindwa kuitambua pia bidhaa aliyotumia awali atakapohitaji kutumia tena, hivyo kuanza kubahatisha.

Kwa kutumia alama ya biashara mteja anaweza kuitambua bidhaa aliyotumia mara ya kwanza kwa kuangalia alama ya bidhaa iliyopo na kuinunua tena kwa mara nyingine tena.

**KUTANGAZA BIDHAA/HUDUMA**

Alama za biashara au huduma zina mchango mkubwa katika kuitangaza biashara au huduma fulani, hasa katika matangazo ya michoro na maandishi, lakini kwa matangazo mengine ambayo huwa sio ya moja kwa moja.

Matangazo haya mara nyingi hujitokeza katika filamu, mabango, vipeperushi, au nyimbo, mara kadhaa unaweza kuwa umeshuhudia nembo fulani inajitokeza katika nyimbo au filamu mathalani katika kinywaji au duka, hii ni aina fulani ya kutangaza biashara.

Hivyo kuwa na nembo ambayo imesajiliwa inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa sana katika kuifanya bidhaa au huduma iweze kufahamika kwa umma.

KUFIKA SEHEMU YA BIASHARA/HUDUMA

Siku zote katika maeneo ya biashara, msongamano wa biashara za aina moja, kwa hali hii wakati mwingine inakua vigumu kwa wateja kutambua sehemu ya biashara ambayo wanakwenda.

Katika mazingira haya pale nembo inapotumika humsaidia mteja kuweza kutambua sehemu ya biashara anayokwenda na kufika kwa urahisi. Hii kwa kiasi kikubwa inasaidia kuongeza idadi ya wateja wanaofika katika eneo lako.

**KUIPA HADHI BIASHARA/HUDUMA**

Katika kutoa huduma au kuuza bidhaa, wateja hugawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na mpango wa mauzo wa mtu au kampuni husika.

Mara nyingi kuna baadhi ya wateja kabla ya kununua bidhaa au kupata huduma wanaangalia hadhi ya bidhaa au huduma na mara nyingi kuna baadhi ya watu hawawezi kabisa kununua au kutumia bidhaa za aina fulani kwa sababu ya hadhi yake.

Katika hali hii nembo ina mchango mkubwa sana katika kuipa hadhi na mwonekano wa kipekee bidhaa au huduma inayotolewa, na pia kumwezesha mteja kufanya maamuzi sahihi kulingana na ubora wa bidhaa au huduma fulani inayotambulishwa na nembo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (Brela), Geofrey Nyaisa.

**KINGA YA KISHERIA DHIDI YA BIASHARA YAKO**

Ni muhimu kuilinda kisheria biashara yako dhidi ya washindani au waharibifu wa biashara za wengine. Mara kadhaa imejitokeza kwamba mtu au kikundi cha watu wanazalisha bidhaa zenye ubora wa chini kwa kutumia nembo ya bidhaa nyingine au kutoa huduma hafifu kwa nembo ya sifa na hadhi sehemu fulani.

Pindi bidhaa hizi ziingiapo sokoni, huharibu sifa nzuri ya bidhaa iliyokuwapo awali. Lakini kama nembo yako ya bidhaa au huduma imelindwa basi inakua ni vigumu kwa wao kutumia nembo hiyo.

Kwa upande mwingine, kuendesha biashara kwa kutumia nembo ambayo haijasajiliwa, mshindani anaweza kuisajili nembo hiyo na kuwa yake bila pingamizi kwa sababu nembo hiyo kisheria haina mmiliki.

Endapo mtu atatumia nembo iliyosajiliwa kisheria basi mmiliki anaweza kumchukulia hatua za kisheria kwa kwenda mahakamani kudai fidia ya matumizi yasiyo halali ya nembo yake na hasara aliyopata kwa udanganyifu huo.

**JE, UNAWEZAJE KUSAJILI ALAMA YAKO YA BIASHARA AU HUDUMA?**

Kwa Tanzania alama ya biashara au huduma (nembo) zinasajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Huduma (BRELA) chini ya Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura ya 326. Taratibu zote za Usajili zinafanyika kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya HYPERLINK "http://www.brela.go.tz" \t "_blank" www.brela.go.tz hivyo haina haja ya kufika katika ofisi za BRELA kwa ajili ya usajili.

Ili kukamilisha usajili, mwombaji atatakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha utaifa kutoka NIDA ambayo itakayomwezesha kufungua akaunti katika mfumo wa usajili na kisha kuandaa ombi la usajili na kuliwasilisha BRELA kwa njia ya mtandao.

Jumla ya gharama kwa ajili ya usajili ni Sh. 130,000 ambayo inalipwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza mwombaji atalipa Sh. 65,000 ambayo ni ada ya ombi pamoja na kutangaza nembo kwa umma ili kujiridhisha kama nembo hiyo haina mmiliki mwingine.

Awamu ya pili mwombaji atalipia Sh. 65,000 ambayo ni ada kwa ajili ya cheti cha usajili baada ya ombi la usajili kukamilika. Muda wa usajili wa nembo ni miezi mitatu ambapo mwombaji atapata cheti cha usajili na kuimiliki nembo yake kisheria.

Katika hiyo miezi mitatu ya usajili kuna takwa la kisheria la kutangaza kwa siku sitini alama "nembo" hiyo kwenye jarida la BRELA linalotoka bure kila mwezi, jarida hilo linapatikana kwenye tovuti ya BRELA.

Kisheria alama ya biashara au huduma ukomo wake ni pale mmiliki wa alama "nembo" hiyo atakapoamua kuacha kutumia kwa kuitaarifu BRELA kupitia kwa Msajili wa Alama za Biashara na Huduma. Sheria ina takwa la kuhuisha nembo hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka saba na baada ya hapo itakuwa kwa kipindi cha kila baada ya miaka kumi.

Alama ya Biashara na Huduma "nembo" ni mali kama zilivyo mali nyingine na zina thamani kubwa sana katika biashara, hivyo ni vema wafanyabiashara wa aina zote wakasajili alama zao za biashara ili kulinda "nembo" hizo zisichukuliwe na maharamia wa biashara.



Mitamba ya ng'ombe wanaopatikana shamba la mifugo la Sao Hill.

# SHAMBA LA MIFUGO SAO HILL KUONGEZA UZALISHAJI MITAMBA

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA ya mifugo ni miongoni mwa chache ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza pato la Taifa. Mpaka kufikia mwaka 2019, sekta hiyo imechangia kwa asilimia 7.4, baada ya ukuaji wake kuongezeka kwa kasi ya asilimia tano.

Kwa kutambua mchango huo serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliamua kuwekeza katika mashamba makubwa ya mifugo ili kuyapa uwezo wa kuzalisha mifugo bora itakayosaidia kukuza uchumi wa nchi na wananchi kwa ujumla.

Moja ya shamba ambalo serikali imewekeza ni la Sao Hill, lilipo kijiji cha Itulavanu, Kata ya Ikongorisi mkoani Iringa.

**ILIPOTOKA SHAMBA LA SAO HILL**

Akielezea safari ndefu ya shamba hilo, Kaimu Meneja, Mtama Gerald Galusi, anasema kuwa lilianzishwa mwaka 1967 baada ya serikali kulitaifisha kutoka kwa wakulima wa kizungu.

Meneja huyo ansema kuwa mwaka 1968, shamba hilo lilianza kufanya kazi rasmi na kutumika kama sehemu ya kuzalisha mitamba bora 'breeding unit' na kuwauzia wafugaji wadogo wadogo wa Nyanda za Juu Kusini.

Galusi anaeleza kwamba Sao Hill imekuwa na uzalishaji mzuri kwa sababu shamba hilo linafaidika na hali ya hewa nzuri ya baridi, ambayo inawafanya mifugo kustawi vyema na kutoa uzalishaji mzuri tofauti na mashamba mengine ambayo yapo katika ukanda wa joto.

Anasema shamba hilo pia linafaidika na Mto Ruaha, ambao maji yake yanatiririka vipindi vyote vya majira kuelekea kwenye bwawa la Mtera.

**MAFANIKIO YA SHAMBA TANGU KUANZISHWA KWAKE**

Akizungumzia mafanikio ya shamba hilo ambalo hadi sasa lina ng'ombe 1,600, meneja huyo anasema wamefanikiwa kuzalisha mitamba mingi na kuisambaza kwa wafugaji wadogo kwa bei nafuu.

Mitamba hiyo imewanufaisha wafugaji wa wilaya zote za mikoa ya Iringa na Mbeya.

Akizitaja baadhi ya wilaya hizo ni Rungwe na Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Busokelo, zimefaidika na utaratibu wa 'kopa ng'ombe lipa ng'ombe,' uliosababisha wananchi wengi kuwa na ng'ombe wa maziwa.

Anaendelea kusema kuwa shamba hilo limezalisha eneo la malisho pamoja na mbegu za majani kwa ajili ya kuwauzia wafugaji wadogo wa kimkoa kwa gharama nafuu.

Galusi anasema ng'ombe kutoka Sao Hill wanapatikana kwa bei nafuu ambayo mfugaji mdogo anaweza kumudu, akitolea mfano Mtamba mwenye mimba anauzwa kwa shilingi 1,600,000, tofauti na mashamba ya watu binafsi ambayo inafikia kati ya 3,000,000 na 4,500,000.

Aidha, meneja huyo ameipongeza serikali kwa kuwajali na kuwapa wafugaji mitamba bora kwa bei ambayo kila mtu anaweza kununua.

**CHANGAMOTO ZINAZOKABILI SHAMBA HILO**

Galusi anasema katika kila mafanikio hapakosi changamoto, hivyo matatizo yanayolikabili shamba hilo ni uchache wa vitendea kazi, hususan usafiri wa kutembelea maeneo ambayo ina mifugo.

Changamoto nyingine ni kuwa eneo hilo lina mvua nyingi ambazo husababisha kupungua kwa madini joto ambayo ni muhimu kwa mifugo, jambo ambalo linawalazimu kununua madini hayo kwa bei kubwa.

**MATARAJIO KATIKA UZALISHAJI**

Kwa upande wa matarajio, Galusi anasema hadi kufikia mwezi Juni, 2020 wamepanga kusambaza mitamba aina ya Borani kati ya 120 hadi 130, kutokana na uhitaji wa ng'ombe hao kuwa mkubwa.

Anasema mitamba hiyo dume aina ya Borani inasaidia kuboresha uzalishaji kwa ng'ombe wa asili kwa wafugaji wadogo wadogo.

Wito kwa Wadau wa Mifugo

Meneja huyo anatoa wito kwa wadau wa Mifugo wazalishe kwa tija ili wawe na maziwa na nyama za kutosha ili kujenga uwezo wa kusambaza kwenye viwanda ambavyo vinachakata mazao ya mifugo.

Pia, aliwashauri wafugaji kutumia mashamba ya serikali kupata madume bora ili waboreshe mifugo yao pia kuitumia kama mashamba darasa ya kujifunzia.

Anaendelea kuwashauri wadau kutumia njia ya uhimilishaji kwani inasaidia kuboresha kosaafu za ng'ombe, ambao wanakuwa haraka tofauti na ukuaji wa ng'ombe wa asili.

Robert Semaganga, Ofisa Mifugo ambaye ni mratibu wa sekta ya ng'ombe wa maziwa, ameishukuru serikali kwa kuanzisha na kuwekeza katika shamba la Sao Hill, kwani limekuwa msaada mkubwa kwa wafugaji.

Akitolea mfano, Semaganga, anasema "Kuna shamba la Justine Bimbiga ambaye ana ng'ombe 54, ambao wengi ni zao la shamba hili, hii inafurahisha kuona mfugaji kuonyesha matokeo bora ya Sao Hill. Pia wanafunzi wa vyuo mbalimbali hufika hapo kujifunza kwa vitendo," anasema Semaganga.

Jobisho Mkonyi, mfugaji wa ng'ombe wa maziwa wilayani Mufindi, anasema kuwa uwepo wa shamba la Sao Hill, kumewasaidia kupata mitamba kwa bei nafuu, ambapo mtamba aliyekuwa anauzwa 1,600,000, sasa anapatikana kwa 1,200,000. Kiasi kilichobaki wamepunguziwa kama ofa kwa wafugaji.

Anaongeza kwa kusema uwepo wa shamba hilo kunawafanya wapate huduma za wataalamu wa mifugo kirahisi na karibu.

Aidha, aliiomba serikali kuendelea kuwasaidia ili waendelee kupata ng'ombe walio bora zaidi ambao wanatoa maziwa mengi.

**USHAURI WA SERIKALI KUHUSU MALISHO**

Mkurugenzi wa Idara ya Malisho, Dk. Asimwe Rwiguza, anasema wafugaji wengi bado wanategemea malisho ya asili ambayo kimsingi hayatoshelezi na hayana viini lishe vya kutosha.

Amewahimiza wafugaji kuandaa mashamba ya malisho na kutumia mbegu bora zinazopatikana kwenye mashamba ya serikali ili kuboresha lishe za mifugo yao.

Aanasema wizara kupitia Idara ya Malisho na Uendelezaji wa Rasilimali za Mifugo, imeendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji na utunzaji wa malisho.

**FAIDA ZINAZOPATIKANA KUPITIA MIFUGO**

Kulingana na Wizara ya Mifugo, ufugaji wa ng'ombe bora una faida nyingi kiuchumi, kwani licha ya nyama na mbolea, humpatia mfugaji nishati ya kupikia ya gesi inayojulikana kitaalam kama 'Biogas'.

Nishati hii ya gesi inapatikana kutokana na kinyesi cha ng'ombe ambacho wengi wanaita samadi.

Wafugaji wakielimishwa na kuhamasishwa vizuri kutumia njia hii mbadala ya matumizi ya nishati ya gesi inayotokana na samadi, inapunguza matumizi ya kuni ambayo kwa muda mrefu sasa serikali imekuwa ikiyapiga vita kwa kuharibu mazingira.

Mfugaji na mkulima kutoka kijiji cha Igowole, Michael Mhosole, aliwaambia maofisa habari wa wizara hiyo, waliomtembelea kuwa ng'ombe aliowapata kutoka Sao Hill, wamemuinua kiuchumi kwa kuuza maziwa ya kutosha na kutumia gesi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Anasema anapata nishati hiyo ya gesi baada ya kujenga mtambo unaotumika kuchakata samadi ya ng'ombe na kuibadilisha kuwa nishati ya gesi tayari kwa matumizi ya kupikia.

Mhosole anasema kuwa nishati ya gesi inayotokana na ng'ombe ikitumika vizuri inasaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

"Pamoja na samadi kunizalishia gesi, pia naitumia kwa ajili ya kurutubisha udongo katika mashamba yangu," anasema Mhosole.

Aidha, anatoa wito kwa wafugaji wenzake kuweka juhudi katika kutunza mifugo yao vizuri kwa kuwapatia huduma zinazohitajika, ikiwamo kuandaa mashamba ya malisho na chakula cha kutosha katika kipindi cha kiangazi ambacho kunakuwa na uhaba.

# Facebook yaondoa matangazo kampeni Donald Trump

**WASHINGTON, Marekani**

KAMPUNI ya mtandao wa kijamii ya Facebook, imefuta matangazo ya kampeni ya Rais wa Marekani, Donald Trump, baada ya kuonekana yana alama zilizokuwa za utawala wa kinazi wa Ujerumani.

Facebook imesema hatua hiyo imechukuliwa baada ya matangazo hayo kuwa na alama ya pembe tatu ya rangi nyekundu, ambayo ilikuwa ikitumiwa na utawala wa kinazi kwa ajili ya kuwatambua wapinzani wao wenye mlengo wa Ukomunisti.

Matangazo hayo yalikuwa ni sehemu ya kampeni ya Trump katika uchaguzi uliopangwa kufanyika mwezi Novemba mwaka huu.

Timu ya kampeni ya Trump, ilijitetea kwamba tangazo hilo lilikuwa linakilenga kikundi cha wanaharakati wa mrengo wa kushoto Antifa, ambacho wanadai kinatumia nembo hiyo.

Katika yaliyotolewa na Mkuu wa Sera za Ulinzi wa Facebook, Nathaniel Gleicher, alisema matangazo hayo yanaenda kinyume na sera yake ya kudhibiti kueneza chuki.

"Haturuhusu alama ambazo zina simama kwa mirengo au kundi linalohamasisha chuki, labda iwe ni kukemea jambo hilo," alisema.

Gleicher, aliongeza "Hicho ndicho tulichokiona kwenye tangazo hili, na popote pale alama hiyo itakapotumika tutachukua hatua kama hii."

Matangazo hayo, ambayo yaliwekwa kwenye kurasa za mtandao wa Facebook za Trump na Makamu wake Mike Pence, yalifutwa baada ya kuwa mtandaoni kwa saa 24.

Aidha, msemaji wa timu ya kampeni ya Trump, Tim Murtaugh, pembe tatu ya rangi nyekundu ni alama inayotumiwa na kundi la Antifa, hivyo ilitumika katika tangazo kuhusu kukosoa kundi hilo.

"Natambua kama Facebook wana kibonzo (emoji) cha pembe tatu nyekundu pia ambacho ni sawa kabisa na tuliyotumia sisi," alikosoa Murtaugh.

Siku za hivi karibuni kiongozi huyo wa Marekani, alilishutumu kundi la Antifa kwa kuanzisha maandamano ya vurugu nchini humo kufuatia kifo cha Mmarekani mweusi George Floyd ambacho kilisababishwa na kukandamizwa shingo na polisi.

Rais Trump, alitishia mwezi uliopita kulitangaza kundi hilo linalopingana na itikadi za kifashisti kuwa kundi la kigaidi la ndani ya nchi. Hata hivyo wataalamu wa sheria hawana uhakika kama ana uhalali wa kufanya hivyo.

***BBC***



Mtoto Melissa Kabore (4), akiruka kwenye dimbwi la maji jirani na machimbo ya kokoto kwenye mji wa Ouagadougou, nchini Burkina Faso. Katika mji huo watoto hucheza kwenye vifusi vya machimbo ya mawe wakati wazazi wakifanya kazi ya kupasua mawe. (**PICHA: REUTERS**)

## Kenya yashinda kiti Baraza la Usalama Umoja wa Mataifa

**NEWYORK, Marekani**

KENYA imeibuka na ushindi dhidi ya Djibouti, katika mchuano wa kuwania kiti cha uwakilishi katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Ushindi wa Kenya umepatikana katika duru ya pili, baada ya hatua ya awali iliyofanyika siku ya Jumatano, kutopatikana taifa lolote lililoweza kupata theluthi mbili ya wingi wa kura katika wanachama 193 wa Umoja wa Mataifa.

Awamu ya pili Kenya, ilipata kura 129 na Djibouti 62.

Kutokana na ushindi huo, nchi hiyo itaungana na Norway, Ireland, India na Mexico. Mataifa hayo yalichaguliwa katika upigaji wa kura wa Jumatano.

Nchi zote zilizochaguliwa hazina uanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, na zitashikilia nafasi hiyo kwa muda wa miaka miwili kuanzi Januari Mosi.

***DW***

## China yakabiliwa na mlipuko mpya corona

**BEIJING, China**

CHINA inakabiliwa na mlipuko mpya, baada ya kuripoti visa vipya 32 vya virusi vya corona katika mji wake mkuu wa Beijing.

Kuibuka kwa wimbi jipya la maambukizi imesababisha serikali kufanya jitihada ya kuyatenga maeneo mengine na mji huo ambao wiki iliyopita watu 183 waliathirika. Kati ya watu waliothibitika kuambukizwa Covid-19, 25 wanatoka Beijing, wawili Jimbo la Hebei na mmoja Liaoning.

Taarifa zinaeleza, visa hivyo vinatokana na mwingiliano wa watu kutoka majimbo ya Guangdong na Gansu. Kutokana hali hiyo, safari zote za mabasi kutoka majimbo mengine, kuelekea Beijing zimesitishwa, huku mamia ya safari za ndege pia zimesimamishwa.

***DW***

# Jogoo aliyeshtakiwa kuwapigia kelele wanandoa afariki

**PARIS, Ufaransa**

DUNIANI kuna vituko! Kuku aina ya jogoo anayeitwa Maurice, ambaye alishtakiwa kwa kosa la kupiga kelele kutokana na kuwika kila siku asubuhi, amekufa baada ya mwaka mmoja tangu ashinde kesi yake.

Jogoo huyo ambaye ana umri wa miaka sita, alishtakiwa mwaka 2019 kwa kudaiwa kuwapigia kelele kila siku wanandoa wastaafu ambao walikwenda kisiwa cha Oleron, nchini Ufaransa kwa ajili ya mapumziko.

Mmiliki wa jogoo huyo, Corinne Fesseau, alisema mashtaka hayo yalifunguliwa akiwa amekosa kutokana na jogoo wake alikuwa akiwika kama wafanyavyo wengine.

Hata hivyo jogoo Maurice pamoja na watu waliomshtaki, hawakufika mahakamani wakati mahakama ikisikiliza kesi hiyo.

Hata hivyo, jogoo huyo alipata umaarufu kimataifa kwa wanaharakati kumfanya kama nembo ya kulinda sauti nchini Ufaransa.

Wanandoa hao Jean-Louis Biron na Joëlle Andrieux, walimlalamikia Fesseau, kuwa alianzisha mabishano baada ya kupewa taarifa na kusababisha mgogoro.

Fesseau, na wafuasi wake ambao ni wanajamii wa mji wake, walitetea kwamba jogoo ni sehemu ya maisha ya watu wa vijijini na mtu hawezi kumnyamazisha.

Mwaka jana, mahakama ilitoa uamuzi wa kumwachia huru jogoo Maurice, baada ya kuonekana hana hatia na alitakiwa kuishi kwa uhuru katika kisiwa cha Oléron.

Jogoo huyo alikufa mapema mwezi huu, huku mmiliki wake akasubiri muda wa kutangaza kifo chake.

"Niliwaza kwamba kwa sababu kuna hatua za kutotoka nje, watu tayari wana mengi ya kukabiliana nayo, na hatutaweza kutangaza kifo kwa sasa," alisema Fesseau wakati akizungumza na kituo kimoja cha redio.

Aliongeza "Tumenunua jogoo mpya na huyu pia tumemwita Maurice, naye anawika kama yule wa kwanza tu. Lakini hawezi kuwa kama Maurice wetu".

***BBC***

# HADITHI

# Mauaji Harusini-17

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Tangu alipokutana na Eddy na maneno yake, kuna kitu ambacho alihitaji kutoka kwake. Alihitaji kuwa naye angalau saa mbili ili aangalie kuna nini ndani yake.

"Sawa, sasa utakuja lini?"

"Kwanza hujaniambia unaishi wapi?"

"Kwa sasa nipo Mbweni."

"Kwa baadaye utakuwa wapi?"

Swali hilo lilimtatiza na kuchekesha Shani na kujiona ni kama alijibu vibaya.

"Baba yangu ana nyumba nyingi hapa mjini. Kuna wakati nakuwa nipo Kigamboni, kwenye nyumba mpya ambayo ndiyo aliyokuwa anakwenda kuishi na mkewe, lakini kuna nyumba yetu nyingine Kigamboni. Huku ndiyo nimechagua nikae mimi kwa sasa. Siwezi kukaa Kigamboni kutokana na lile tukio lililotokea." Alijibu kwa unyenyekevu.

"Nimekuelewa. Leo si Ijumaa? Nitakuja Ijumaa ijayo?"

"Mbona mbali hiyo jamani?" Shani alilalamika.

"Najua. Lakini vumilia tu. Mambo mazuri hayataki haraka."

Shani alikubaliana na Eddy na kukata simu. Akaibusu.

"Mambo mazuri gani tena hayo." Alijisemea mwenyewe baada ya kukata simu.

Kwa mara ya kwanza Shani alijiona kwenye furaha zaidi kuliko wakati mwingine wowote ule.

Aliwaza jinsi atakavyotembelewa na mwanaume jasiri, mwenye kujiamini, mchangamfu na mcheshi kwa jinsi tu alivyomuona.

"Itakuwa ni siku ya furaha sana." Alisema kwa sauti. Lakini ndani alikuwa peke yake. Wafanyakazi wake wawili, wa kike na wa kiume walikuwa nje wakiendelea na shughuli zao.

*********************************

Gari aina ya Toyota Brevis yenye rangi nyeusi iliingia kwenye geti la jumba kubwa la kifahari la marehemu Patiyo lililopo maeneo ya Mbweni jijini Dar es Salaam.

Baada ya kuingia geti lilifungwa. Aliyekuwa anaendesha gari hakuwa mwingine ila ni Eddy Kamal.

Aliteremka na kupokewa kwa bashasha na mwenyeji wake Shani. Hakujizuia kumkumbatia.

"Hujambo mrembo?" Alisalimia huku akiwa amekumbatiwa na mwenyeji wake "Sijambo, karibu nyumbani. Maana hata siamini kama umekuja." Alisema Shani akiwa amemng'anga'ania mgeni wake.

"Ni mwanaume wa ajabu tu ambaye anaweza kuitwa na msichana mrembo kama wewe, asije." Alijibu.

Ilikuwa ni kama sinema ya bure kwa wafanyakazi wake wawili wa kike na wa kiume, ambaye kwa mara ya kwanza walishuhudia bosi wake akiwa mwenye furaha, akikumbatiana na mwanaume.

Hata wao waliangaliana na kutabasamu.

Muda mfupi tu baada ya maongezi yao, Shani aligundua kuwa anaongea na mtu mwenye upeo wa hali ya juu.

Awali alijua tu ni mwanaume mchangamfu, mwenye kujiamini, lakini alichogundua ni kwamba anaelewa vitu vingi mno ambavyo si kawaida kwa mtu mwingine kuvijua.

"Kuna vitu nataka unisaidie." Shani alimwambia Eddy akimtazama kwa wizi.

"Naweza kama vinaweza kukusaidia."

"Mimi natarajia kukabidhiwa mali zote za marehemu baba yangu, majumba, mashamba, makampuni na biashara zingine alizokuwa nazo kwa sababu mimi ndiyo nilikuwa mtoto wake pekee."

"Enhee, sasa hapo mimi nahusika na nini Shani?"

"Unajua mimi nimeshatokea kukuamini na kukuona mwenye akili nyingi sana. Nataka nikuajiri kazi uwe msiamizi mkuu. Kwa sababu mimi pamoja na kwamba ni msomi, lakini ni mwanamke, tena msichana mdogo, kuna sehemu nitakwama, nitahitaji mtu kama wewe, unasemaje?"

Eddy alitabasamu kiasi cha kumshangaza Shani. Alichukulia kama ni jambo ambalo litamshtua Eddy, lakini aliona kama analichukulia mzaha.

"Nitakupa mshahara unaoutaka Eddy?" Shani alimbembeleza.

"Mshahara?" Eddy alishtuka.

"Ulichokisahau ni kwamba hata kama nitakubali kusimamia, basi nitasimamia mali za mjomba wangu na shangazi, sasa kwa nini nidai mshahara?"

Ni jibu lililomuacha hoi Shani. Hakujua acheke, atabasamu au afanya nini. Akabaki kimya.

"Shani, kwani si una ndugu za baba yako, hakuna hata mmoja anayeweza kusimamia mali hizi ila mimi tu?"

Swali hilo lilionekana kumkasirisha kidogo Shani.

"Eddy, mimi kukwambia wewe uwe msimamizi, siyo kwamba sina ndugu wa baba au mama. Ninao. Na wapo waliosoma wenye uwezo wa kusimamia, lakini binafsi sitaki yoyote yule ajihusishe na mali hii. Na si kwa sababu mimi ni mchoyo na nitawanyima misaada, hapana. Kila watakachokuwa wanataka mimi nitawapa na hasa ndugu wa baba yangu. Lakini ninachotaka ni mimi kuwa salama na hizi mali." alisema kwa sauti iliyoonekana ya ukali kidogo.

**"Unajua mimi nimeshatokea kukuamini na kukuona mwenye akili nyingi sana. Nataka nikuajiri kazi uwe msiamizi mkuu. Kwa sababu mimi pamoja na kwamba ni msomi, lakini ni mwanamke, tena msichana mdogo, kuna sehemu nitakwama, nitahitaji mtu kama wewe, unasemaje?"**

"Kama wewe hutaki sema tu."

"Kwa hiyo niache kazi zangu?"

"Si liniambia huna kazi wewe."

Ni kweli, Eddy alikumbuka kuwa alimwambia hana kazi yoyote ile siku ile walipokutana makaburini.

"Halafu siyo kama kazi itakuwa kubwa sana, ni usimamizi tu, kwa sababu kila kitu kinajiendesha.

Baba aliacha kila kampuni ikiwa inajiendesha, ina wafanyakazi na viongozi wake, hapa kinachotakiwa ni usimamizi tu na ufuatiliaji wa pamoja, kati ya mimi na wewe." Shani alizidi kusisitiza.

"Nimekuelewa Shani hili jambo linazungumzika. Siyo kama ninakuzungusha kukubali. Ni kwamba kwa kufiwa na baba yako mzazi, akikuacha bado msichana mdogo unayetarajia kubeba majukumu makubwa ambao huna uzoefu nayo, ni lazima upate msaada mkubwa sana. Kama wapo baadhi watakaokupa msaada huo, na mimi nitakuwa mmoja wa watakaokupa kampani, wala usihofu." Alisema na kumuondoa hofu Shani.

Baada ya kumaliza maneno mazito, walibadilisha maongezi na kuanza yale yanayomfanya Shani awe na furaha.

"Hivi humu kweli unalala peke yako kweli?" Eddy aliuliza kimzaha.

"Ulitaka nilale na nani?"

"Mmmmh, nauliza tu, maana binti nzuri kama wewe kuwa huna mwenyewe kweli?"

"Sina mtu yoyote Eddy. Siyo kama watu hawagongani. Yaani ni balaa. Matajiri rafiki za baba, vijana wao, mamaneja wa makampuni, mawaziri, wabunge, wameshatupa ndoana we, lakini mimi nimewatolea nje."

"Kwa nini mtoto mzuri kama wewe unawatolea nje na unaishi peke yako, bila hata mtu wa kukuliwaza?"

"Kwanza umri wangu bado mdogo miaka 23 kwa hiyo sina papara sana. Muda upo. Nataka nitafakari kwanza kwa kina. Ninampata nani na ananitaka kwa nini?"

"Na mimi binamu yako pia hunitaki?" Eddy alimuuliza kwa mara nyingine kwa utani.

Shani aliangua kicheko, kwa sababu hakutarajia swali kama hilo.

"Umeanza hivyo?"

"Ndiyo, shangazi yangu na baba yako baada ya kufunga ndoa si wamekufa pamoja na kuzikwa pamoja, mmoja kushoto, mwingine kulia?"

"Ndiyo unataka kusemaje?"

"Na mimi na wewe mmoja awe kushoto na mwingine kulia."

*Itaendelea Jumamosi*

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**LIKINJIYE SAMUEL NGUYAINE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba P.1619-0091** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **VICTORY SEKONDARI** mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/GOG/RB/464592/2020.**

215782202

## KUPOTEA KWA CHETI



**BONAVENTURA NTAGAMBI MAZEZELE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.151/14 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SENGEREMA SEKONDARI mwaka 1984. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/466231/2020.**

215782302

## KUPOTEA KWA VYETI



**Theodosia John Komba** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1163/0147** kikichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari Ujenzi, Cheti cha shahada/certificate chenye **LGTI/BTCCP/2015/322** kilichotolewa na Chuo cha Local Government Training Institute mwaka 2016, Cheti cha Diploma chenye namba **LGTI/DSP/DCD/2016/0189** kilichotolewa na Chuo cha Local Government Training Institute mwaka 2017. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/460964/2020**

215781502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MIKOANI TRADERS LTD** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 734 CWR TOYOTA IST.** Rangi ya kijani. Chassis namba **INZA737719.** Engine namba **NCP810041819.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KBA/PS/B.1/29/VOL.XXIV/**

115782702

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**( DODOMA DISTICT REGISTRY)**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3 OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late ABISAI GODSON LYIMO of Dodoma Municipality/ City at Itega**

**AND**

**In the matter of the application for letters of Administration by ANNA DONALDI MMARI**
**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of July 2020.
Date at Dodoma this 16 Day of JUNE 2020.

DEPUTY REGISTRAR

115782402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;158/2020**

**Ombi la REHEMA SELEMANI KISASILE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu KARUME ALLY MIRAMBO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/06/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI

115782102

**IN THE RESIDENT COURT OF TANZANIA**
**AT TANGA**

**CIVIL APPEAL NO. 4/2020**

**SWAHIBU SANGIWA.......................................APPEALLANT**

**VERSUS**

**NGOKA SINGO CHAMBUA & OTHERS...............RESPONDENTS**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TO: 1. ALLIANCE INSURANCE CORPORATION LTD**
**2. AMRAN NASSORO ALLY**

**TAKE NOTICE THAT,** the Appellant instituted an appeal against you with particulars set out on an appeal filed in this court. Service of the summons on you has been ordered by means of this publication. You are directed to collect copies of the summons and appeal from the courts Registry P.O. Box 97, Tanga. Your are hereby summoned to appear in this court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 25/06/2020 at 9:00am when this appeal will be mentioned.
**TAKE NOTICE THAT** should you default to enter appearance in court on the day and time mentioned above, the appeal will proceed and judgment may be given in your absence.
GIVEN under my hand and the seal of the court this 15th day of June, 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

215781702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;149/2020**

**Ombi la JESSEPHINE JACKSON KATEGILE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JACKSON AUGUSTINO KATEGILE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/06/2020.

215782002

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose*

*Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# Benzema: Sikuwaza kuwa ndani ya tano bora Madrid

**MADRID, Hispania**

KARIM Benzema kamwe hakuwahi kufikiria kama angekuwa miongoni mwa wafungaji bora watano wa Real Madrid baada ya kuizima rekodi ya Ferenc Puskas, Alhamisi.

Mshambuliaji huyo alifunga mara mbili wakati Madrid iliporudi kupitwa pointi mbili na wapinzani wao ambao vinara wa LaLiga, Barcelona wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Valencia.

Benzema alimwondoa Puskas (mwenye mabao 242) katika nafasi ya tano na kuishika yeye kwenye orodha ya wafungaji wa wakati wote wa Madrid akifikisha mabao 243, nyuma ya Cristiano Ronaldo (451), Raul (323), Alfredo Di Stefano (308) na Santillana (290).



Mfaransa huyo ambaye aliwasili pale Madrid kutoka Lyon mwaka 2009, alikuwa na furaha kubwa kufikia mafanikio hayo.

"Sikuwahi kufikiria kitu kama hiki, nina furaha sana. Nimekuwa nikifanya kazi kwa muda mrefu sasa na mara zote najiimarisha mwenyewe," alisema Benzema kupitia tovuti ya klabu hiyo.

"Natumaini naweza kuendelea. Nina furaha kuendelea kuichezea klabu hii."

Bao la pili la Benzema mwenye umri wa miaka 32 alilofunga kwa kuunganisha pasi nzuri ya Marco Asensio na kumfunga golikipa wa Valencia, Asper Cillessen.

Benzema amefunga mabao 21 katika mechi 38 msimu huu, huku Madrid itarudi tena uwanjani dhidi ya Real Sociedad Jumapili.

# MOURINHO:

## SPURS HAIWEZI KUSHINDANA KWENYE USAJILI

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amekubali Tottenham Hotspur haiwezi kushindana na timu zinazotumia fedha nyingi kwenye usajili wa Ligi Kuu England kama wapinzani wao Chelsea na Manchester United.

Spurs ilivunja rekodi yake ya usajili Julai mwaka jana wakati ilipotumia kiasi cha pauni milioni 55 kumsajili, Tanguy Ndombele kutoka Lyon, huku Giovani Lo Celso, Steven Bergwijn na Ryan Sessegnon kwa pamoja walinunuliwa kwa jumla ya pauni milioni 100 misimu miwili iliyopita.

Hata hivyo, Mourinho hataraji Spurs kutumia fedha nyingi tena wakati dirisha la usajili litakalofunguliwa, licha ya kuona wiki hii Chelsea wakikubali kulipa pauni milioni 47.5 kwa usajili wa Timo Werner atakayetua Julai na tayari wamefikia makubaliano na Ajax kumsajili Hakim Ziyech.

"Kila timu inapambana na hali yake na falsafa yake," amesema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Sitarajii kuwa kwenye nafasi ya kufanya usajili mkubwa. Natarajia klabu kuwa na uwiano na hilo ndilo tunalolifikiria.

"Tunajua kwamba tunakwenda kwenye ligi ile ile, huku klabu nyingine zikipambana kutumia fedha nyingi kwenye usajili.

"Tuna mifano tayari jinsi klabu zinavyowekeza, sisi hatuwezi kushindana kwenye soko la usajili na bado tuna mechi tisa kumaliza msimu."

# Ozil atacheza akiwa fiti, asema Arteta

**LONDON, England**

MIKEL Arteta atamchagua tena Mesut Ozil kuichezea Arsenal hadi wakati atakapoamini kuwa mchezaji huyo anaweza "kuwa kwenye ubora wake" dimbani baada ya raia huyo wa Ujerumani kuondolewa kwenye mchezo dhidi ya Manchester City.

Ozil kwa mshangao aliachwa kwenye kikosi cha washikabunduki hao Jumatano wakati wakichezea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa City, ukiwa ni mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu tangu mlipuko wa virusi vya corona.

Kiungo huyo wa zamani wa Real Madrid hakuwapo hata kwenye orodha ya wachezaji wa akiba.

Arteta awali alikuwa akimtumia mara kwa mara mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 tangu alipochukua nafasi ya ukocha hapo kwenye dimba la Emirates.

"Nimekuwa muwazi sana kwa Mesut tangu siku ya kwanza. Tangu nilipojiunga, nilifikiri kwamba alikuwa fiti na alikuwa tayari kucheza na nilitaka acheze katika kiwango chake cha juu kabisa," amesema Arteta akiwaambia waandishi wa habari Alhamisi.

"Alicheza kila mechi na mimi, nafikiri. Ndio hivyo. Wakati nitakapoona kwamba yupo tayari tena kucheza, nilimchukulia kama mchezaji mwingine yoyote.

"Nafikiri nimekuwa muungwana sana kwake, na alionyesha kiwango nilichokitaka kwenye mechi nyingi."

## HABARI MICHEZO




# JUVE KUWAKOSA SANDRO, KHEDIRA

**TURIN, Italia**

JUVENTUS inajiandaa kurudi kwenye Ligi Kuu Italia bila, Alex Sandro na Sami Khedira wakati watakapokuwa wakipigania kubeba taji la Serie A kwa mara ya tisa mfululizo, wakianza na Bologna, Jumatatu.

Mlinzi wa kushoto, Sandro aliumia goti wakati Juve wakifungwa na Napoli kwenye fainali ya Coppa Italia, Jumatano.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil imeripotiwa kwamba matatizo yake hayo ya goti yanaweza kumweka nje ya dimba kwa kipindi cha wiki tatu.

Khedira aliumia nyama za paja wakati wa kujifua kuelekea mchezo wa fainali pale dimba la Olimpico, ambapo Napoli walishinda kwa penalti 4-2 baada ya dakika 90 kumalizika bila kufungana.

Juve haikuweka wazi wawili hao watakaa nje kwa muda gani ili kurejea uwanjani kuendelea na majukumu yao.

Taarifa ya klabu hiyo ilisema: "Uchunguzi wa madaktari unaonyesha kwamba Alex Sandro, aliumia goti na ameshaanza matibabu haraka.

"Kwa upande wa Khedira, aliumia nyama za paja. Kwa siku chache zijazo tutajua kwa muda gani watahitaji kurudi uwanjani."

## KANE, SON FITI KUIVAA UNITED

**LONDON, England**

HARRY Kane ataanza kwenye kikosi cha Tottenham Hotspur dhidi ya Manchester United akitoka kuwa majeruhi kwenye mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu England tangu mlipuko wa virusi vya corona, kocha Jose Mourinho amethibitisha.

Kane mwenye umri wa miaka 26, aliumia Spurs wakati wakifungwa 1-0 na Southampton mwaka mpya, na kumfanya kuwa nje ya dimba kwa kipindi kirefu.

Awali iliripotiwa kwamba ataukosa msimu wote uliobaki, lakini kutokana na ligi kusimama baada ya mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona kwa miezi mitatu, mfungaji huyo wa Spurs alipata nafasi ya kupona na sasa anarudi uwanjani kumalizia mechi tisa zilizobaki.


Moussa Sissoko (aliyeumia goti) na Son Heung-min (aliyevunjika mkono) pia walitarajiwa kuwa nje ya dimba kwa msimu wote, lakini wamerudi mapema.

Wakati akizungumza kuhusu habari hizo Alhamisi, Mourinho alisema: "Tuna majeruhi wachache, lakini tutasubiri hadi kesho (jana Ijumaa) kabla ya kujua kama watacheza au la.

"Bila shaka (Japhet) Tanganga aliumia miezi michache iliyopita na hajapona kwa wakati.

"Lakini wale waliofanyiwa upasuaji kama Kane, Son na Sissoko, hawa watatu wamepona kabisa na wapo tayari kucheza."

"Kane hajacheza soka kwa zaidi ya miezi sita, hivyo amejifua vya kutosha. Naweza kuwaambia kwamba Kane hana tatizo na ataanza kwenye mchezo dhidi ya Manchester United."




# PSG yajitosa kumwania Alaba



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain, imetangaza vita ya kuwania saini ya mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba, ikimtazama kama mbadala sahihi wa Thiago Silva, atakayeondoka klabuni hapo mara baada ya msimu huu kumalizika.

Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Leonardo amethibitisha kuwa wataachana na Silva katika msimu wa usajili wa majira ya joto na wanamtazama Alaba kama mbadala wake sahihi.

Mkataba wa Alaba kwa sasa umebakiza miezi 12 na baada ya miezi sita atakuwa huru kusaini makubaliano ya awali na timu nyingine kwani kanuni za usajili zinaruhusu.

Lakini ripoti zinadai kwamba PSG, hawahitaji kusubiri hadi muda huo ufike ili wampate mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 27, hivyo wanafanya jitihada zote kuhakikisha wanaipata saini yake katika usajili wa nyakati za kiangazi baada ya ligi msimu huu kumalizika.

Alaba ni moja ya wachezaji ambao wana uwezo mkubwa wa kushambulia na kuzuia kwa wakati mmoja tofauti na mabeki waliopo PSG kwa sasa ambao wamekuwa na ufanisi kwenye eneo moja tu.

Ingawa Bayern wenyewe wameweka wazi kuwa hawana mpango wa kumuuza mchezaji huyo, lakini hawatakuwa na nguvu ya kumbakisha ikiwa atalazimisha kuondoka kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake.

Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, Hasan Salihamidzic, mapema wiki iliyopita alinukuliwa akieleza namna wanavyotamani kumwona mlinzi huyo akibaki ndani ya kikosi chao siku za usoni.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# CHELSEA YASUBIRI KUMSAJILI HAVERTZ

●●● Ni kwa sababu dau la mshambuliaji huyo litashuka endapo Leverkusen itashindwa kukata tiketi ya ...

**LONDON, England**

CHELSEA huenda ikamsajili kwa dau dogo mshambuliaji, Kai Havertz kama klabu yake ya Bayer Leverkusen itashindwa kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, vyombo mbalimbali vimeripoti.

Klabu hiyo ya Stamford Bridge inaendelea na kujiimarisha katika mchakato wa kuwania saini za wachezaji mbalimbali ikisubiri kufunguliwa kwa dirisha la usajili hapo Alhamisi, huku ikiwa ikikaribia kumsajili Timo Werner kutoka RB Leipzig, na tayari imemnasa, Hakim Ziyech.

Kwa sasa bado ilikuwa katika changamoto ya kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Havertz baada ya kuelezwa kwamba Leverkusen inataka kulipwa pauni milioni 90 ili kumuuza mshambuliaji huyo.

**Lakini Football.London imeandika kuwa kama klabu hiyo haitafuzu kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu ujao, thamani yake itashuka rasmi.**

Kikosi hicho kinachoongozwa na Frank Lampard kilikuwa tayari kumnunua mshambuliaji huyo kwa dau la pauni milioni 70, na Leverkusen itakuwa tayari kumuuza kwa dau hilo kama itakosa tiketi ya kushiriki michuano hiyo ya kimataifa.

Kwa sasa bado wako katika mbio za kusaka tiketi hiyo, wakiwa kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, maarufu Bundesliga.

Leverkusen ina pointi moja tofauti dhidi ya Borussia Monchengladbach ikiwa na mechi mbili mkononi za Bundesliga, huku wakitofautiana kwa bao moja na klabu iliyoko katika nafasi ya tano.

Havertz na wachezaji wenzake watakutana na Hertha Berlin na baadaye Mainz katika mechi zao mbili za mwisho wakati Monchengladbach yenyewe itawakabili Paderborn halafu Hertha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Leverkusen, Fernando Carro amethibitisha Havertz ataondoka klabuni hapo kama atahitaji kufanya hivyo.

"Klabu mbalimbali zinamwitaji mchezaji huyo," kiongozi huyo aliliambia gazeti moja la Ujerumani liitwalo Kölner Stadt-Anzeiger. "Ninaona wachezaji wanahitaji kusonga mbele wakati fulani ili kupata changamoto mpya."

"Lazima ifike wakati uheshimu uamuzi wao na kwa kuzingatia ukweli mkataba wake unamalizika ifikapo 2022."

## KWA UFUPI

### LUIZ, ARSENAL KUTETA

MKATABA wa beki, David Luiz amesema na Arsenal unatarajiwa kumalizika ifikapo Juni 30, mwaka huu na hatima ya Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 33 itajulikana wikendi hii. Inaelezwa mchezaji huyo anataka kusaini mkataba wa miaka miwili. **(Talksport)**

### ARTETA AMCHAMBUA OZIL

KOCHA Mikel Arteta amefunguka kuwa kiungo Mjerumani, Mesut Ozil, ambaye ana umri wa miaka 31, hayuko tayari kuendelea kuichezea klabu hiyo. **(Times - subscription required)**

### KANTE NJIA NYEUPE

CHELSEA iko tayari kumuuza kiungo Mfaransa N'Golo Kante (29), ili kusaidia kutunisha mfuko wa fedha wa klabu hiyo kwa ajili ya kuhakikisha straika wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (24), kutoka RB Leipzig anatua klabuni kwake. **(Times - subscription required)**

### LEVERKUSEN NJIA PANDA

MABOSI wa Bayer Leverkusen wamesema kwa sasa wanamuuza Kai Havertz kwa dau la pauni milioni 90, lakini endapo watashindwa kufuzu kucheza fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya, thamani ya nyota huyo itashuka na kufikia kiasi cha pauni milioni 70, ambazo Chelsea wako tayari kulipa. (Football.London)

### RODGERS AMTAJA CHILWELL

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers amesema nyota wa Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell hana ulazima wa kuondoka Foxes kwa lengo la kutaka kuendeleza kiwango chake na kuwa mmoja wa mabeki bora duniani, lakini hana uhakika kama beki huyo anayehusishwa na Chelsea atabakia. **(Guardian)**

### POGBA BADO YUPO

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, Peter Schmeichel amesema "watu sahihi" wamemweleza kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (27), anataka kubakia Old Trafford. **(Express)**

### INTER YAMGANDA SANCHEZ

MABOSI wa Inter Milan wako katika mazungumzo na Manchester United kuhusiana na uwezekano wa kumbakisha kwa mkopo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Chile, Alexis Sanchez (31), katika msimu ujao. **(Sky Italia - in Italian)**

### ARSENAL, UNITED VITANI

ARSENAL na Manchester United zimeonyesha nia ya kuwania saini ya winga wa Roma, Cengiz Under (22), thamani ya nyota huyo wa timu ya Taifa ya Uturuki ni pauni milioni 27. **(Corriere dello Sport, via Mail)**

### COUTINHO KUBAKIA BAYERN

BAYERN Munich imekubali kuongeza mkataba wa kiungo mchezeshaji Mbrazil Philippe Coutinho (28), ambaye yuko kwa mkopo akitokea Barcelona mkataba wake wa awali unamalizika Juni 30, mwaka huu na hivyo ataichezea mechi za mwisho za Ligi ya Mabingwa Ulaya hapo Agosti. **(Sky Germany)**

### BELLINGHAM AJIONGEZA

MANCHESTER United imeshangazwa na taarifa zilizoandikwa na vyombo mbalimbali vya Ujerumani kuwa kiungo wa Birmingham City, Jude Bellingham amechagua kujiunga na Borussia Dortmund kwa sababu atapa uhakika wa kucheza wakati wote. **(Soccernet)**

### VALENCIA YAMTAKA CEBALLOS

VALENCIA imeweka wazi inahitaji kunasa saini ya kiungo, Dani Ceballos. Mhispania huyo ambaye yuko kwa mkopo Arsenal akitokea Real Madrid, anaonekana kama anaweza kuondoka katika klabu hiyo ya Emirates mkataba wake utakapomalizika. **(Marca)**

HABARI MICHEZO

# MBAO FC YAFUNGWA MECHI SITA MFULULIZO

**Na Adam Fungamwango**

HALI imekuwa mbaya kwa Mbao FC ili kusalia katika Ligi Kuu Bara kutokana na mwenendo wao mbovu, ilipopoteza kwa mara ya sita mfululizo kwenye mechi yao ya Jumapili dhidi ya Azam FC kwa mabao 2-0, Uwanja wa Azam Complex Chamazi jijini Dar es Salaam.

Timu hiyo inayokamata nafasi ya 19 kati ya timu 20 zinazoshiriki Ligi Kuu, ikiwa na pointi 23, imeshindwa kupata ushindi tangu Februari 18, mwaka huu ilipoichapa Singida United mabao 3-1 kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba.

Baada ya hapo imekuwa ikiambulia vipigo mfululizo vinavyoiweka kwenye hali ngumu kubakia kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Rekodi zinaonyesha ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, CCM Kirumba, Mbao iliambulia kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Mwadui FC, Februari 22 mwaka huu, kabla ya kuzabuliwa mabao 2-0 Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani dhidi ya Ruvu Shooting, Februari 29, mwaka huu.

Vipigo viliendelea kwa Mbao, kwani kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam ilijikuta ikichakazwa mabao 3-0 dhidi ya Yanga, mechi iliyochezwa Machi 3, na Machi 7, mwaka huu ilipata kipigo kingine cha mabao 2-0 dhidi ya KMC, Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Mbao FC ilikwenda kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kuambulia kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mbeya City Machi 10, kabla ya ligi kusimama kupisha ugonjwa wa Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona, lakini mechi ya kwanza tu iliporejea ikaambuliwa kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Azam FC.

Timu hiyo itashuka tena dumbani siku ya Jumatano kwenye Uwanja wa CCM Kirumba kucheza dhidi ya Coastal Union kuona kama inaweza kufurukuta na kubaki Ligi Kuu.

Mbao ilipandishwa Ligi Kuu mwaka 2016 na Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF), na kuzishusha daraja timu nne za Geita Gold, Polisi Tabora, JKT Kanembwa na JKT Oljoro kutokana na kupanga matokeo.



Beki wa Yanga, Deus Kaseke (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa JKT Tanzania, Abdallah Waziri katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma Jumatano. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Namungo, Kagera Sugar zatambiana

**Na Saada Akida**

MAKOCHA wa Namungo, Thierry Hitimana na Mecky Maxime wa Kagera Sugar, kila mmoja ametamba kikosi chake kitafanya vema katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa mkoani Lindi.

Namungo itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kupata pointi moja ugenini dhidi ya Coastal Union baada ya sare ya mabao 2-2, huku Kagera Sugar ikiwa ni mechi yao ya kwanza tangu kurejea kwa ligi hiyo iliyokuwa imesimama kupisha janga la corona.

Hitimana aliweka wazi katika mechi hiyo atamkosa mshambuliaji wake, Blaise Bigirimana ambaye ni majeruhi, huku Reliants Lusajo akirejea uwanjani baada ya kukosekana katika mchezo uliopita kutokana na kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano.

Aliongeza anawaheshimu Kagera Sugar kwa sababu ni moja ya timu nzuri zinazoshiriki Ligi Kuu Bara na imejipanga kusaka matokeo chanya ili kufikia malengo yao.

Naye Maxime alisema kikosi chao kipo vizuri na tayari wamejipanga kurejea na pointi tatu muhimu katika mchezo huo wa leo.

"Vijana wangu wapo fiti, tunawaheshimu Namungo ni timu nzuri na ipo katika nafasi ya juu katika msimamo, lakini kwetu pia hatupo tayari kuona tunapoteza alama muhimu katika mchezo huo," alisema Maxime.

Aliongeza mechi zote za ligi zina changamoto kwa sababu kila upande unashuka uwanjani ukiwa na malengo tofauti.

## Mkutano Mkuu DOREFA kufanyika leo

**Na Somoe Ng'itu**, DODOMA

CHAMA cha Soka Mkoa wa Dodoma (DOREFA), kinatarajia kufanya Mkutano Mkuu wa mwaka leo jijini hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa DOREFA, Khamisi Kissoyi, alisema maandalizi ya mkutano huo yamekamilika na wajumbe wote wameshawasili jijini hapa tayari kwa kushiriki kikao hicho.

Kissoyi alisema wanaamini mkutano huo utapitisha na kujadili ajenda mbalimbali kwa maslahi ya maendeleo ya soka ya Dodoma na si vinginevyo.

"Ni kweli tuko katika maandalizi ya mkutano mkuu, ni mkutano mkuu wa mwaka lakini utakuwa na mambo mengi ya msingi, hata tukielekea kwenye uchaguzi," alisema kiongozi huyo.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Soka la Wanawake Dodoma (DWFA), Tatu Said alisema chama chake kitahudhuria mkutano huo na kimejipanga kuhakikisha kinatetea maslahi ya wanawake.

"Mimi maswali yangu yatakuwa ni yanayohusu soka la wanawake, Dodoma tunahitaji kuwa mbele pia kwenye soka, tunataka mambo yaendelee na yasirudi nyuma, naamini viongozi wetu wataungana na sisi," alisema Tatu.

Alisema baada ya kumalizika kwa mkutano huo, ndio kalenda mpya ya mashindano ya ligi ya wanawake itajulikana sambamba na kuacha kwa mchakato wa uchaguzi wa kupata viongozi wapya.

## Zimamoto kamili kuivaa Mlandege

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

UONGOZI wa Zimamoto umesema kikosi chao kiko imara na tayari kuwakabili Mlandege katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa Juni 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Zimamoto, Ali Jongo, alisema imefanya maandalizi mazuri na iko tayari kukabiliana na ushindani watakaokutana nao katika mchezo huo.

Jongo alisema wanaamini ushindi katika mchezo huo utawasaidia katika mbio zao za kuwania taji la Ligi Kuu Zanzibar.

"Wachezaji wetu wapo tayari kuendelea na ligi ambayo tupo katika hatua ya mwisho, ninaamini kila timu imejipanga kuonyesha ushindani na kuhakikisha inajiweka mahali salama na kubaki Ligi Kuu," alisema Jongo.

Kiongozi huyo ametaka vilabu vinavyotishia kugoma kuendelea na ligi hiyo kwa sababu ya ukata kuacha mawazo hayo kwa sababu wadau wote wa soka wakiongozwa na wachezaji wanaelewa changamoto hiyo iliongezeka kutokana na ugonjwa wa corona.

Alipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Rais wao, Dk. Mohammed Shein kwa jitihada za kusaidia soka visiwani humo na kuthamini mchango walioutoa na kueleza hoja za kususia ligi hazina msingi.

Michezo
Jumamosi Juni 20, 2020
Nipashe



Chelsea yasubiri kumsajili Havertz HABARI UK 22



Beki wa Simba, Kennedy Juma (kushoto) akiwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa timu hiyo, Rashid Juma katika mazoezi ya kujiandaa na Mwadui FC, katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA, MWADUI MECHI YA KISASI

●●●Imejipanga kurekebisha makosa ya mchezo wa kwanza, na kuvuna pointi tatu muhimu zitakazowasogeza kwenye...

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi, Simba wanatarajia kuwakaribisha 'wababe' wao Mwadui FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kuanzia saa 10: 00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Mwadui FC ikiwa mwenyeji katika mechi ya mzunguko wa kwanza, ilikuwa timu ya kwanza kuwafunga vinara hao wa Ligi Kuu Bara ikiibuka na ushindi wa bao 1-0, shukrani kwa mshambuliaji wake Gerald Mdamu, huku ikiondolewa kwa 'taabu' kwa matuta kwenye michuano ya Kombe la FA.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, alisema timu yake imejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na amewataka wachezaji wake kusahau matokeo ya mchezo wa kwanza dhidi ya wapinzani wao hao.

Sven alisema wamejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo huo na kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za kuwania taji hilo la Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema anajua mechi hiyo itakuwa ushindani kwa sababu wachezaji wake hawatakubali kuona wanapoteza tena dhidi ya Mwadui, huku wageni hao wakicheza bila presha kutokana na kuvuna pointi tatu walipokuwa nyumbani kwao.

"Utakuwa ni mchezo mgumu na wenye changamoto, lakini nimewaandaa wachezaji wangu kuutizama mchezo wa kesho (leo), na kuacha kufikiria matokeo yaliyopita, tunahitaji kuongeza pointi ili kukaribia kile tunachokifikiria, malengo yetu ni kuchukua ubingwa wa ligi," Sven alisema.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema mechi ya leo inatarajiwa kuwa ngumu lakini kikosi chake kiko kamili kuondoka na pointi tatu muhimu za mchezo huo.

"Kikosi kiko kamili, wachezaji wana ari, tunakutana na Mwadui ambao ni moja ya timu bora, tumejipanga kupata pointi tatu mbele ya wapinzani wetu, utakuwa mchezo mgumu ila tupo tayari kwa ajili ya kupambana na maandalizi yapo sawa," alisema Rweyemamu.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema ushindi wa mechi ya leo ni muhimu kwa sababu utawasaidia kuendelea kujiimarisha katika mbio za ubingwa na endapo watashindwa, watakuwa hawapo makini kwenye safari ya kutetea taji hilo wanalolishikilia.

"Matarajio yetu ni kupata pointi tatu, wachezaji wanalijua hilo, benchi la ufundi linafahamu, tunahitaji mashabiki waje kwa wingi ili kunogesha ushindi, kesho (leo), katika mechi ya kesho (leo), hatujui matukio matatu (sare, ushindi, kufungwa), tunahitaji tukio moja la kupata pointi tatu tu, sio tukio lingine," alisema Manara.

Khalid Adam, Kocha Mkuu wa Mwadui, aliliambia gazeti hili wamejiandaa vizuri na mechi ya leo na kikubwa wataingia kwa tahadhari kwa sababu wanajua wapinzani wao watacheza kwa presha.

"Hatuna wasiwasi na mechi hii, vijana wangu wako vizuri, ninaitambua Simba ni timu nzuri, tunajuza uzuri na mapungufu yao, tutaongeza umakini, wasitarajie kupata pointi tatu," Khalid alisema.

Simba itashuka katika mchezo wa leo ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ruvu Shooting, wakati Mwadui yenyewe ilichapwa goli 1-0 na Yanga.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Coastal Union dhidi ya Mtibwa Sugar wakati KMC FC itawakaribisha Ruvu Shooting, huku Lipuli FC wakiwafuata Polisi Tanzania, JKT Tanzania itavaana na Singida United na Ndanda FC itachuana na Biashara United kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa Yanga kuwakaribisha Azam FC kuanzia saa 1:00 kwenye Uwanja wa Taifa.

## YANGA, AZAM FC TAMBO ZATAWALA

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, akisema malengo yao ni kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mechi yao dhidi ya Azam FC, mabingwa hao watetezi wa Kombe la FA, wametamba jeshi lao liko kamili kusaka pointi tatu muhimu.

Hata hivyo katika mchezo huo, Yanga itamkosa beki wake tegemeo, Lamine Moro ambaye alionyeshwa kadi nyekundu katika mechi iliyopita dhidi ya JKT Tanzania, wakati Azam itashuka dimbani bila nyota wake muhimu wa kikosi cha kwanza wakiwamo Waghana watatu ambao wamekwama nchini kwao.

Eymael aliliambia gazeti hili wachezaji wake wamejiandaa kufanya vizuri katika mechi ya kesho na michezo yote iliyobakia ya msimu huu ili malengo yao ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Bara yatimie.

Mbelgiji huyo alisema matokeo ya sare waliyopata katika mechi iliyopita dhidi ya JKT Tanzania hayajawarudisha nyuma na kusisitiza mipango yao ya kutafuta nafasi ya pili, iko pale pale.

"Tunaendelea na mazoezi kuelekea mchezo wetu ujao dhidi ya Azam, mechi itakuwa na ushindani mkubwa sababu wote tunahitaji pointi muhimu, wapinzani wetu wanahitaji kujiimarisha kuendelea kubaki katika nafasi ya pili hali na sisi tunahitaji kuifikia nafasi hiyo," alisema Eymael.

Alisema wachezaji wake wako vizuri akiwamo mshambuliaji, Bernard Morrison na Papy Tshishimbi aliyekuwa majeruhi ambao wanatarajia kurejea katika mchezo huo.

"Nitaangalia utimamu wa mwili wa Morrison, endapo atakuwa fiti ninaweza kumtumia nyota huyo, tunahitaji kumaliza ligi katika nafasi ya pili na vile vile kutwaa ubingwa wa Kombe la FA, tunafanya kazi mapungufu yanayojitokeza, nimewakumbusha pia kutumia vema nafasi za kufunga wanazozitengeneza," Eymael alisema.

Ofisa Habari wa Azam FC, Zaka Thabit, alisema jana timu yake imekamilika na inamejipanga kusaka matokeo mazuri dhidi ya wapinzani wao katika mchezo huo.

"Jeshi liko kamili, tumejipanga kupata ushindi, tutawakosa nyota wetu kadhaa akiwamo Domayo (Frank) na nyota wetu Waghana, waliobaki wako sawa na tayari kwa mchezo," alisema kiongozi huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >